**PROFESA** Janabi awa kivutio kijijini kwake, apokewa kwa shangwe na wananchi

UKURASA 4

**NCHIMBI** amkumbuka Hayati Mkapa kumwezesha Shahada ya Uzamili

UKURASA 4

**MTUHUMIWA** akutwa amejinyonga hadi kufa ofisi ya kijiji

UKURASA 8


Nipashe Spotika

10 - BORA YA USAJILI WA MAJIRA YA JOTO HADI SASA UK. 12

MAKIPA WA4 WA KUMRITHI EDERSON MANCHESTER CITY

ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Julai 29, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581752

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


LIKE & FOLLOW US


# HOMA YA INI TISHIO

UKURASA 3

## BAADHI YA DALILI

1. Uchovu
2. Kichefuchefu
3. Mwili kuwa dhaifu
4. Homa kali
5. Kupoteza hamu ya kula
6. Kupungua uzito
7. Maumivu makali ya tumbo upande wa ini
8. Macho na ngozi kuwa vya njano
9. Mkojo mweusi





Dk. Grace Maghembe, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya

**RIPOTI MAALUM:**

# Ukeketaji wageuzwa kipato

**MALIPO** ya ngariba 20,000/- hadi 40,000/- kwa kichwa... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **DJUMA AIBUKIA NAMUNGO FC** UK 23

**MAONI, KATUNI UK.6**

RIPOTI MAALUM

# Ukeketaji wageuzwa kipato

## -Malipo ya ngariba 20,000/- hadi 40,000/- kwa kichwa

**Na Elizabeth Zaya aliyekuwa**
TARIME



Mkurugenzi wa Sauti ya Jamii Kipunguni- Ukonga jijini Dar es Salaam, Selemani Bishagazi, akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Mpakani Sirari mkoani Mara kuhusu namna ya kuachana na mila kandamizi. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

MAPATO makubwa wanayopata ngariba na wazee wa mila wakati wa sherehe za ukeketaji yanasababisha vita dhidi ya ukatili huo kuwa ngumu.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe wilayani Tarime, mkoani Mara hivi karibuni, umebaini ngariba hulipwa wastani wa Sh. 20,000 hadi 40,000 kwa kila msichana anayemkeketa, baadhi wakikeketa wasichana 150 hadi 200 kwa siku wakati wa msimu wa sherehe hizo za kimila.

Mwandishi wa Nipashe amebaini sherehe hizo hufanywa mwishoni mwa mwaka, zikichukua muda wa wiki mbili hadi tatu. Hivi sasa sherehe hizo zinafanywa katika miaka inayogawanyika kwa mbili tu.

Hata hivyo, sheria za Tanzania zinakataza kufanya utekeketaji na adhabu yake ni kifungo cha hadi miaka 15.

Ngariba Wankyo Chacha, mkazi wa Kijiji cha Mpakani, Kata ya Sirari, wilayani Tarime anathibitisha amekuwa analipwa kwa kufanya ukeketaji, malipo ambayo hugawana na wazee wa mila.

"Ni kweli kuna malipo unapofanya kazi hii, lakini sisi (ngariba) huwa tunasikiliza na kutekeleza maagizo ambayo tunapewa na wazee wetu wa mila kwa sababu wao ndio viongozi katika koo, wanaheshimika toka enzi na enzi.

"Na hata kile kinachopatikana baada ya kazi huwa ni lazima kigawanywe sawa kwa wazee wa mila na ngariba kwa kuwa wao ndio waratibu wakuu wa kazi hii," anasema Wankyo.

Ngariba huyo ambaye anadai hajui kwamba anavunja sheria kwa kukeketa wasichana, anataja changamoto kubwa kwake baadhi ya watoto kuogopa na hivyo kujikuta anatumia muda mrefu tofauti na unaopangwa na wazee wa mila.

"Unaweza kuletewa mtoto ambaye ni mwoga, kila ukitaka kumfanyia, analia. Hivyo, inabidi utulie uzungumze naye kwanza. Ukikutana na watoto wengi wa namna hiyo wanakupotezea muda, badala ya kukeketa 150 kwa siku, unajikuta umekeketa 100 au badala ya kumaliza kazi ndani ya wiki mbili unajikuta unakwenda hadi wiki tatu au zaidi.

"Gharama ya kufanya kazi hiyo kwa kila mtoto ni Sh. 20,000, kwa siku unaweza kuwafanyia watoto 100 au 150, unapata fedha nyingi," anasema Wankyo.

Mmoja wa wazee wa mila katika Kijiji cha Nyamrenge, Kata ya Sirari, Francis Mwita, anatetea ukeketaji katika jamii yao kwa maelezo kwamba mafundisho ambayo huambatana na shughuli hiyo ya ukeketaji yanasaidia kujenga wasichana katika maadili mema.

"Suala la tohara tuwaachie wazee, wenyewe ndio watajua watamaliza vipi, lakini ukiliingilia unaokosea. Huko wasituguse kabisa kwa sababu ndio mila tuliyozaliwa nayo na tumerithi kutoka kwa wazee wetu.

"Watoto kukeketwa kuna maana tatu: Mtoto wa kike kabla ya kukeketwa, bibi zake huwa wanamwambia hatakiwi kutembea na mwanamume kwa sababu akifanya hivyo siku, akienda kukeketwa hatakeketwa kwa sababu atajulikana kwamba tayari ameshatembea na mwanamume na analeta aibu katika familia.

"Pili, akishakeketwa anaambiwa asikumbatiwe na mwanamume wala kuguswa kwenye kifuani kwa sababu akifanya hivyo, kuna miiko ambayo hatafanyiwa akigundulika. Kwa hiyo, inasaidia ajilinde.

"Tatu, anaambiwa akishaolewa hatakiwi kutembea nje ya ndoa kwa sababu kutokana na miiko aliyofanyiwa atagundulika. Hiyo miiko inasaidia watoto kuwa na maadili.

"Hivyo, tunashauri serikali itafute njia nzuri ya kumaliza hili polepole na si harakaharaka kama wanavyotaka.

"Hii nguvu inayotumika kutaka kuzuia watoto kukeketwa itachangia wawe huru zaidi kufanya mambo ya ajabu kwa sababu wanafahamu kwamba hata wakifanya hivyo, hakuna mtu atajua lakini endapo wataendelea kukeketwa wataizidi kuogopa na hawataharibikiwa," Mzee Mwita anasema pasi na kuzingatia ukeketaji unakiuka sheria za nchi na ni ukatili dhidi ya wasichana.

Ester Wambura (21), mkazi wa Forodhani, kijijini Mpakani, Kata ya Sirari anasimulia alivyolazimishwa kukeketwa na wazazi wake, akidai walimtishia kwamba asipokeketwa, angetengwa na asingepata mwanamume wa kumuoa.

"Nikiwa darasa la sita, wazazi wangu waliniambia ninatakiwa kukeketwa, binafsi sikutaka lakini wazazi waliniambia ni lazima kwa sababu nitatengwa na itakuwa aibu kwa familia na wakanitishia sitapata mwanamume wa kunioa, hivyo nikakubali.

"Baada ya kukeketwa alijitokeza mwanamume anataka kunioa hata kabla sijamaliza elimu ya msingi. Kwa kutaka kuwaridhisha wazazi wangu, sikutaka kufanya vizuri hata kwenye mitihani yangu ya darasa la saba ili niolewe, lakini ninapoisimulia haya leo, nina watoto wawili na mume ameniacha.

"Ninajutia uamuzi wangu, ninatamani nisingekeketwa labda hao wanaume wasingeshawishika kunifuata na ningeweka nguvu zangu kwenye masomo na huenda ningekuwa na maisha mazuri baadaye," Ester anajuatia uamuzi wake.

Elizabeth Joseph, mkazi wa Kijiji cha Bondeni, Sirari, anasema haamini kama kweli ukeketaji kwa sasa upo kwa ajili ya mila, bali kwa maslahi ya watu, akiwa na hoja kwamba wapo wanawake waliokeketwa katika ya eneo anamoishi, lakini wameachwa na waume zao, kama ilivyo kwa mtangulizi wake - Ester.

"Tunasema wanaendekeza ukeketaji kwa sababu hivi sasa hatuwaelewi wanaume, wanataka wanawake wakeketwe lakini wakiwaona hao waliofanyiwa hivyo, hawawataki tena. Tuna ushahidi wa wanawake wengi waliokeketwa ambao wameachika, wanasema wanataka wanawake wasiokeketwa.

"Tunataka serikali iongoze nguvu kukemea jambo hili lisifanyike kabisa kwa sababu kuna watu wanaangalia maslahi yao wenyewe wakati watoto wanaumia. Binafsi nimekataa watoto wangu wasikeketwe, ninataka wasome kwa uhuru mpaka wachoke wenyewe," anasema Elizabeth.

Msichana aliyekimbia kukeketwa mwaka 2020 (jina tunalo), anasema kuwa hadi sasa wazazi wake hawataki arejee nyumbani na anaishi. Hivi sasa msichana huyo (17) analelewa katika kituo kinachopokea watoto waliokimbia kukeketwa kilichoko wilayani Serengeti, mkoani Mara.

"Mimi nilikimbia wakati maandalizi yote yameshafanyika na siku iliyokuwa inafuata, nilitakiwa nifanyiwe, wazazi walikuwa wamenunua kila kitu kwa ajili ya sherehe na watu walikuwa wamealikwa.

"Sikuonesha dalili yoyote ya kukataa wala kuwaabishia, nilikubali huku moyoni nikipanga namna ya kukimbia. Huwezi amini, alfajiri sana kama saa 10 hivi, nikajifanya kama ninawahi kudamka kwa ajili ya maandalizi, kumbe ndio ninatoroka.

"Nguo nilizobeba hazikuzidi tatu na nilizipitisha dirisha la nyuma ya nyumba. Nikatokea mlangoni, nikiwa nimebeba ndoo kama ninakwenda kuchota maji, nikazunguka nyuma ya nyumba kuchukua hizo nguo na ndoo nikaiacha palepale, nikaondoka taratibu kwa kunyata huku nimejitanda kanga mpaka barabarani. Nikapanda bodaboda mpaka hapa kituoni.

"Kipindi hicho nilikuwa ninasoma darasa la saba. Baada ya msimu wa ukeketaji kuisha, Januari 2021 nikapiga simu nyumbani, hawakutana kunisikiliza, nikaenda na mwalimu anayetusaidia hapa, naye hawakumsikiliza.

"Madai yao wanasema aibu niliyosababisha kwa familia ni kubwa. Nikakubaliana na matokeo, nimejifunza ushonaji kwa msaada wa kituo hiki. Sasa ninashona nguo za wateja, ninapata fedha zangu mwenyewe, ninaamini nikipata fedha za kutosha nitaanza kuwasaidia watakubali nirudi nyumbani," anasema.

Rhobi Samweli, Mkurugenzi wa Kituo cha Hope for Girls and Women in Tanzania anakolelewa msichana huyo wilayani Serengeti, anasema baada ya serikali na wadau kuweka nguvu zaidi ya kuzuia ukeketaji, ngariba na wazee wa mila wamebadili mbinu; wanawavalisha watoto wa kike nguo za kiume na kofia na kuwachanganya kundi moja na wavulana wanaopelekwa kufanyiwa tohara kimila.

Mkurugenzi huyo pia anasema ukeketaji unafanyika kwa miaka inayogawanyika kwa mbili tu, wakiamini miaka hiyo inakuwa na baraka, mavuno mengi na haina mikosi.

Rhobi pia anasema kuwa kutokana na kukusanya fedha nyingi, wazee wa mila wakati wa msimu wa ukeketaji hufikia hata hatua ya kukodi ngariba kutoka nchi jirani - Kenya.

"Wanajua ngariba atalipwa kutokana na kazi hiyo. Kwa mfano, kama wamepanga kila mtoto anakeketwa kwa Sh. 40,000, wanaganawana nusu kwa nusu.

INAENDELEA KESHO

HABARI KITAIFA

# Homa ya ini tishio, takwimu zaonesha...

**Christina Mwakangale na Jeniffer Gilla**

TAKWIMU za homa ya ini duniani zinaonesha zaidi ya watu milioni 240 huugua. Tanzania, watu watano hadi wanane kati ya 100 wanaugua ugonjwa huo, hususan aina ya B na C.

Bingwa wa Magonjwa ya Ini na Mfumo wa Chakula kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Tuzo Lyuu, amebainisha hayo jana, jijini Dar es Salaam, katika maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani, ambayo huadhimishwa Julai 28, kila mwaka.

Tovuti ya Umoja wa Mataifa (UN), kwenye maadhimisho hayo jana, imebainisha kwamba homa ya ini inaua takribani watu 3,500 kila siku licha ya kuwapo kinga na tiba, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

WHO inasema kiungo hicho kina shughuli zaidi ya 500 kila siku, kuhakikisha binadamu anaendelea kuishi, likisisitiza umuhimu wa kuchunguza, kutibu na kuzuia virusi vya homa ya ini.

Akifafanua kuhusu ugonjwa huo, Dk. Lyuu alisema kwa kawaida mwili hupambana na ugonjwa huo, iwapo ni homa ya ini aina ya A na E.

"Kuna aina ya homa ya ini katika makundi haya; virusi vya hepatitis A na E na hepatitis B na C. Ugonjwa huu maambukizi yake aidha ni kwa njia ya kujamiiana bila kinga, kuongeza damu ya mwenye homa hii au kwa njia ya mdomo yaani chakula.

Hata hivyo, maambukizi yanaweza kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito. Homa ya ini aina ya A na E huwa haiwi 'chronic' (sugu) na haikai muda mrefu mwili hupambana wenyewe ila wapo ambao hushindwa kupambana," alisema bingwa huyo.

Alisema kuwa homa ya ini ya hepatitis B na C ndiyo hatari na maambukizi hukaa muda mrefu mwilini na yenye kuambukiza zaidi na kwamba duniani takribani watu 650,000 hupoteza maisha kutokana na homa hiyo.

"Dalili za homa hii ni kutapika, macho kuwa ya njano, tumbo kuvimba. Madhara yake ni uvimbe katika ini au kupata saratani. Mabadiliko ya ini kusinyaa na kushindwa kufanya kazi," alisema bingwa huyo.

Kuhusu tiba bingwa huyo alisema anayeugua homa aina C, inashauriwa aanze tiba ambayo kwa asilimia zaidi ya 95 ya wanaotumia dawa wanapona.

**WHO**

WHO inasema chanjo wakati wa utotoni, hupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi sugu na visa vya saratani ya ini na cirrhosis katika utu uzima.

"Ni wakati wa kuchukua hatua, kila sekunde 30 mtu mmoja anafariki dunia kutokana na ugonjwa unaohusiana na homa ya ini.

Lazima kuchagiza hatua bora za kinga, uchunguzi na tiba ili kuokoa maisha na kupata matokeo bora ya afya."

WHO, kimataifa kuna aina tano za Homa ya Ini za virusi vinavyosababisha homa ya ini A, B, C, D na E. Kwa ujumla, maambukizi ya homa ya ini aina ya B na C ndio yamesambaa zaidi na husababisha vifo vya watu milioni 1.3 kila mwaka na maambukizi mapya kwa watu milioni 2.2 kila mwaka.

Licha ya kuwapo kwa mbinu bora za uchunguzi na matibabu na kupungua kwa gharama za huduma hizo, viwango vya uchunguzi na matibabu vimedorora, linasema WHO.

Shirika hilo linaona dunia ina nafasi ya kufikia viwango vya kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030, iwapo hatua zitachukuliwa mapema hivi sasa.

"Watu 6,000 huambukizwa homa ya ini B na C kila siku. Vifo vinavyosababishwa na virusi vya homa ya ini vinaongezeka. Mwaka 2022 homa ya ini aina B na C vilisababisha vifo vya watu milioni 1.3."

Serikali yataka wazazi kuzingatia chanjo kwa watoto

**UMUHIMU CHANJO**

Serikali imewataka wazazi kuwapa chanjo watoto wao wanapozaliwa ili kuwakinga na maradhi ya kuambukiza ikiwamo homa ya ini.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini kitaifa yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam yakiwa na lengo la kuongeza uelewa wa tatizo hilo.

Aliwakumbusha wazazi hao kutotoka hospitali bila watoto wao kupatiwa chanjo, akieleza kwenye chanjo hizo ipo ya homa ya ini na inamkinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

Aidha, serikali ilijumuisha chanjo hiyo tangu mwaka 2002 kwenye chanjo inayojulikana kitaalam kama 'pentavalent vaccine' wanayopatiwa watoto chini ya miaka mitano kuwaweka salama dhidi ya virusi hivyo.

Aliwapongeza Watanzania wanaojitokeza kuchangia damu na kuwahamasisha wengine kuunga mkono kwa kuwa inasaidia kuokoa maisha ya wagonjwa wanayoihitaji ikiwamo homa ya ini, Ukimwi, saratani na waliopata ajali.

Alisema uchangiaji damu pia husaidia serikali kuitambua hali ya maambukizi ya magonjwa hayo kwa kuwa inakwenda kupimwa kuangaliwa usalama kabla ya kuwekewa mgonjwa.

Alisema utekelezaji wa utoaji chanjo ya homa ya ini inatokana na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi na Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCoP), uliozinduliwa na wizara ya afya Novemba, mwaka jana.

Alisema magonjwa mengi yanaweza kuzuilika iwapo Watanzania watapata taarifa sahihi wanapokwenda kufuata huduma.

Watanzania pia wamekumbushwa kuzingatia matumizi sahihi ya dawa na kula milo sahihi kwa kuwa magonjwa mengine ya ini yanatokana na matumizi mabaya ya vitu hiyo pamoja na kemikali.

Mkuu wa Programu wa Wizara ya Afya, Dk. Catherine Joachim, alisema kwa mara ya kwanza nchi hiyo inafanya maadhimisho ya kitaifa ya ugonjwa huo toka mpango wa NashCop ulipozinduliwa Novemba 24, 2023.

Alisema tangu walipoanza kutoa huduma ya kupima ugonjwa huo Julai 25, mwaka huu, idadi ya waliojitokeza kupima hadi kufikia juzi ni 524, kati ya hao 15 sawa na asilimia 2.8 waligundulika kuwa na maambukizi, ambao ipo chini ya kiwango cha ushamiri cha kimataifa ambao ni asilimia tatu.

Watu 429 walipokea chanjo ya kwanza na kuunganishwa na vituo vingine ili wapate chanjo mbili zilizobakia, jumla ya chupa 26 za damu zilikusanywa kutoka kwa wachangiaji na watu 275 walipatiwa huduma ya ukatili wa kijinsia na 114 walipata huduma ya macho.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Profesa Janabi apokewa kwa shangwe kijijini kwake

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

MKURGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, juzi aligeuka kivutio kijijini kwake Mtakanini, Kata ya Msindo wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, ambako na timu yake ya wataalamu walikwenda kutoa huduma za afya.

Wananchi hao walifurahi kumwona mtoto wao ambaye ni maarufu kwa kutoa ushauri wa kutunza afya kwa kula vyakula vinavyofaa na umuhimu wa kufanya mazoezi, huku wakishukuru kwa uamuzi huo na kuomba muda zaidi kwa wataalamu kutoa huduma.

Daktari huyo bingwa ambaye amewahi kuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), ni mzaliwa wa kijiji hicho ambaye elimu yake ya msingi alianzia kijijini hapo.

Prof. Janabi alikwenda kuungana na madaktari bingwa watatu waliokuwa wakiendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa moyo, kisukari, tezi dume na saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa gazeti hili, wananchi hao walisema wamefurahishwa na mtoto wa nyumbani kuwakumbuka na kutumia utaalam wake na wenzake kwenda kuwasaidia.

"Tulimsubiri yeye na wataalam wengine kwa hamu kubwa. Wamekaa nasi kwa wiki moja tunatamani wangeendelea kukaa nasi au kwenda kwenye vituo vingine.

Tunatamani mpango huu uwe endelevu tupate alimu ya afya kama anavyotoa kwa wengine huko aliko," alisema Cartas Nyoni.

"Profesa Janabi ni mwenetu, amekuja kwa muda mfupi tunatamani angekaa muda mrefu ili watu waelewe vizuri, tunawaomba wawe wanatutembelea wakiwa na vifaa vya kisasa kama walivyokuja navyo sasa. Wananchi wanyonge wamepata huduma vizuri na bure wangekwenda kwenye vituo vya afya, hospitali za rufani wangetozwa fedha nyingi, tunaomba huduma kama hizi kwa wananchi tunaoishi vijijini," alisema.

Aidha, wameishuruku Wizara ya Afya na kuomba kusogezewa huduma ya madaktari bingwa kwa watu wanaosumbuliwa na moyo, saratani ya kizazi na tezi dume kwenye vituo vya afya wilayani humo.

Diwani wa Kata ya Msindo Remna Nchimbi alisema kuwa kitendo cha serikali kuwaleta madaktari bingwa toka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kimeleta matumaini makubwa kwa wananchi ambao wamekuwa wakisumbuliwa na magonjwa ambayo yanahitaji kuona na madaktari bingwa kwwa lengo la kupata tiba ambao wako mbali na maeneo ya vijiji.

Diwani Nchimbi aliiomba wizara iangalie uwezekano wa kuwa na mpango endelevu kwa madaktari bingwa ambao wako kwenye hospitali za rufani ikiwamo MNH kufika kila mara kwenye vituo vya afya kutoa huduma kwa wagonjwa ili kupunguza changamoto zinazo wakabili za kufuata huduma hiyo kwenye hospitali za juu.

Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, Vita Kawawa alisema amefurahishwa na kazi nzuri zilizofanywa na madaktari bingwa ambao walianza kazi hiyo ya kuwa huduma wangonjwa wa magonjwa ya moyo, kisukali, saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake na tezi dume.

Alisema Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo na baadaye walikwenda kutoa huduma hiyo kwenye Kituo cha Afya Lusewa pia walitoa huduma kwenye Vituo vya Afya Mputa na Mtakanini na kuleta faraja kwa wananchi.

Aidha, wananchi hao walikuwa wakishindwa kupata tiba kutokana na gharama kubwa ya matibabu ambayo kwa kipindi cha zaidi ya wiki moja imetolewa bure.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mtakanini, Profesa Janabi baada ya kupokewa na mamia ya wananchi, alisema nia ya serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri ya afya kuanzia kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na Hospitali za Rufani ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Profesa Janabi ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya moyo alisema kuwa kila mtu anapaswa kutunza afya yake kwa kula vyakula ambavyo si hatarishi kwa afya ili wnanchi waache kula vyakula bila kufuata utaratibu.

Aidha, alisema ni vyema kuepuka kula vyakula vyenye sukari nyingi kwa kuwa sukari haijawahi kumwacha mtu salama.

# Nchimbi amkumbuka Hayati Mkapa kumwinua kielimu

**Na Gwamaka Alipipi,** MASASI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amefichua Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa alivyomsaidia kujiendeleza kielimu.

Amesema ndiye aliyempatia Shilingi milioni mbili ili akajiendeleze elimu ya juu Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa kusomea shahada ya pili.

Alisema hayo jana mkoani Mtwara baada ya kuweka shada la maua katika kaburi la Rais Mkapa, Kijiji cha Lupaso, wilayani Masasi.

Mkapa alifariki dunia Julai 24, 2020 jijini Dar es Salaam na alizikwa kijijini kwake Lupaso.

Baada ya kuweka shada la maua, Dk. Nchimbi alizungumza na wananchi wa kijiji hicho na kusema (yeye) alikuwa ni mwanafunzi wa kisiasa wa Rais Mkapa.

"Mimi ni mwanafunzi wa kisiasa wa Rais Benjamin Mkapa. Alipokuwa Rais, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana CCM kwa miaka saba. Siku moja nilikutana naye na akaniuliza kiwango cha elimu yangu. Nikamjibu nina shahada ya kwanza."

Alisema alimwambia Rais Mkapa kwamba anatamani kujiendeleza kusoma, lakini hakuwa na fedha.

"Baada ya kumwambia kwamba nina shahada ya kwanza akaniambia haitoshi natakiwa nikasome tena. Nikamjibu fedha ni tatizo. Hivyo, kesho yake akanitafuta akaniambia ana barua yangu. Akaniambia amefuatilia kiwango cha ada katika Chuo Kikuu Mzumbe na kubaini haizidi Shilingi milioni mbili. Akanipatia fedha za kwenda kusoma chuo na nikaenda kusoma."

Dk. Nchimbi alisema miezi sita baadaye akiwa chuoni Rais Mkapa akamtafuta na kutaka kujua maendeleo ya chuo.

"Rais Mkapa alikuwa ni mtu mfuatiliaji sana hususani kwa vijana."

Alisema kitu kilichompa shida na kumsumbua hadi sasa ni kushindwa kuja nchini kuhudhuria mazishi ya Rais Mkapa wakati akiwa Balozi wa Tanzania nchini Brazil.

Alishindwa kuja kwa sababu wakati huo kulikuwa na mlipuko wa ugonjwa wa corona uliosababisha nchi nyingi duniani kufunga mipaka yake.

Aidha, mipaka ya nchi ilipofunguliwa alikuja nchini na moja kwa moja alikwenda nyumbani kwa Hayati Mkapa na kumpa pole mke wa Mkapa, Anna Mkapa.

Dk. Nchini alisema CCM chini ya Mwenyekiti wake Rais Samia Suluhu Hassan itaenzi, kuimarisha mambo mazuri yote yaliyofanywa na kuasisiwa na Hayati Rais Mkapa.

Mkapa enzi za uhai wake ni mmoja ya Watanzania waliotoa nguvu, akili ya kuijenga Tanzania.

**MCHUJO NDANI YA CHAMA**

Alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Masasi, Dk. Nchimbi aliwasisitiza wanachama wa chama hicho kuchagua viongozi wazuri wenye sifa ya kuongoza taifa.

Alisema hivi sasa fedha za serikali zinatafunwa kuanzia juu kabla hazijafika ngazi ya chini, hali inayosababishwa na wanachama wa CCM kuchangua viongozi wasiokuwa na maadili.

Alisisitiza wanachama wa CCM wana wajibu wa kupata viongozi wazuri wenye moyo wa kuwatumikia wananchi.

"Wale wazuri miongoni mwetu wapewe nafasi ya kuongoza. WanaCCM wanajukumu la pekee la kuchujana kuhakikisha wanapata viongozi wazuri ambao wanapata nafasi ya kuongoza jamii ambao tunategemea tukiwapa heshima hiyo wataleta heshima ya CCM na nchi yetu," alisema.

Kadhalika, anaamini umoja na utulivu ulipo nchini unategemea uwapo wa CCM kuwa madhubuti endapo wanachama wake watashikamana, kupendana, kushirikiana na kuhakikisha kuwa wanachama wake wanatambua wajibu wa kuwatumikia Watanzania kwa nguvu zote.

**KUKUBALI MATOKEO**

Akizungumza wilayani Masasi, Dk. Nchimbi aliwataka wanachama wa CCM kukubali matokeo wanaposhindwa.

Alisema kuna baadhi ya wagombea wakishindwa katika uchaguzi wa ndani wanakasirika na wananunua kwa zaidi ya miaka mitano.

"Ukienda kwenye uchaguzi nenda kwa mapenzi ya chama. Ukishindwa nenda ukajipange tena kwa ajili ya uchaguzi ujao. Mimi mwaka 1994 niligombea udiwani nikapigwa (kushindwa) vizuri tu. Nikakubali matokeo. Uchaguzi ukipita tukubali matokeo."

Dk. Nchimbi amenza ziara ya siku sita katika mikoa ya Lindi na Mtwara yenye lengo la kukujenga na kukiimarisha chama.

Katika ziara hiyo Dk. Nchimbi ameambatana na Katibu wa NEC-Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, Katibu wa NEC-Organaizesheni, Issa Ussi Haji (Gavu) na Katibu wa NEC- Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Rabia Abdallah Hamid.

**BANI INVESTMENT LIMITED**
DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS
**TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na BENKI YA CRDB tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali iliyoorodheshwa hapo chini kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MKOPAJI/MMILIKI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| John Emmanuel Kitibu | Nyumba yenye C.T No. 46810-LR Mwanza,L.O.No. 495089,Plot No. 177,Block 'F' | Majengo-Kahama | 15.8.2024 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| Alphonce Augustino Masubo | Nyumba(Deed of security arrangement) | Mbulu Mhongolo-Kahama | 15.8.2024 | 6:00 mchana nakuendelea |
| Thereza Gabriel Mponya | Nyumba(Deed of securtity arrangement) | Lyalu-Bariadi | 24.8.2024 | 4:00 asubuhi |
| Julius Makima Kebasa | Nyumba(Deed of security arrangement) | Buriba-Sirari-Tarime | 31.8.2024 | 4:00 asubuhi |
| Khatwibu Sdru Rajab | Nyumba yenye C.T No 56199-LR Mwanza,L.O No. 462449,Plot 190,Block 'E' | Mukalyambwa -Muleba | 7.9.2024 | 4:00 asubuhi |
| Mahamudu Mohamed Msagula | Nyumba iliyopo kwenye Kiwanja no. 242 | Jida South-Masasi | 7.9.2024 | 4:00 asubuhi |
| Daniel Lucas Mabula | Nyumba(Deed of Security arrangement) | Kizwite-Sumbawanga | 14.9.2024 | 4:00 asubuhi |
| Eliah Noel Maleko | Nyumba(Deed of security arrangement) | Nantacha-Kizwite-Sumbawanga | 14.9.2024 | 6:00 mchana nakuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo" as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713224578, 0673020867, 0768339289, 0713295747**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**ESTHER MATHIAS MAJIGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0778-0568** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SONGE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2020.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Control No. 9910841874390.**

**KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI**

**WILSON BASHIRI KAVISHE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye umiliki wa jina la HEIFER PROJECT INTERNATIONAL TANZANIA yenye namba za usajili MC 234 BCF aina ya HONDA. CHASSIS NUMBER LTMJD2192F530. ENGINE NUMBER JD21E2224422. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/26377/2024.**



Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Warda Abeid (kushoto), akiongoza harambee ya kuchangia ujenzi wa nyumba ya mwalimu wa shule shikizi ya Soito katika kijiji cha Naberera, ambapo zilipatikana Sh. milioni 51.8, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# 'Utekaji' watawala mdahalo wagombea urais TLS

**Na Elizabeth Zaya**

MDAHALO wa wagombea urais Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), umeibua suala la vitendo vya utekaji huku kila mmoja akijinadi kupambana nalo iwapo atachaguliwa.

Mdahalo huo uliandaliwa na Kituo cha Televisheni cha Star TV na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali, mwishoni mwa wiki.

Wanaogombea nafasi hiyo ni Sweetbert Nkuba, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda, Kapteni Ibrahim Bendera, Emmanuel Muga na Boniface Mwabukusi.

Akizungumzia matukio ya utekaji, Nkuba alisema kunapokuwa na tishio kwa jamii, kinachotakiwa kufanyika ni kuchukua hatua thabiti ya kudhibiti matukio hayo.

"Mimi ni mdau wa haki, kwa hiyo suala la utekaji na uhalifu mwingine nakemea kwa nguvu zote. Sio jamii ya kistaarabu inayopaswa kuwa na matukio ya namna hiyo."

Mwabukusi alisema endapo atachaguliwa atahakikisha anazuia siasa katika mambo ya msingi yanayohusu uhai wa watu.

"Lazima watu wawajibike na tuache kufanya siasa kwenye maisha ya watu. Jambo la pili tutaomba Jeshi la Polisi kuwa na usimaizi. Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), asimamiwe, hatuko salama chini ya IGP, kwa 'statement' (taarifa) nilizosikia baada ya utekaji sio za kutakiwa kuvumiliwa hata sekunde moja kwa mtu anayeamini katika suala la utawala bora.

Kuuli alijinadi kwa kusema kutokana na kushamiri matukio ya utekaji, kuna haja ya kuweka mazingira yatakayozuia yasitokee ikiwamo Idara ya Usalama wa Taifa pamoja na Jeshi la Polisi kushirikiana kudhibiti.

"Kunapokuwa na matukio ya namna hiyo ya utekaji na watu kupotea katika mazingira ambayo hayaelewe-ki, tunaamini kwamba kuna haja ya kuweka mazingira ambayo yatazuia matukio kama hayo kutokea, kuna umuhimu wa Idara ya Usalama wa Taifa na Jeshi la Polisi kushirikiana katika hili," alisema Kuuli.

Kaunda alisema, akichaguliwa kuwa rais wa TLS, atashauri iundwe tume ya kijaji ambayo ni huru itakayofanya uchunguzi wa ndani kuhusu matukio hayo.

Suala lingine lililoibuka wakati wa mdahalo huo ni mikataba mbalimbali ambayo serikali imekuwa ikitia saini, ambayo wagombea hao walisema kuna haja ya TLS na viongozi wake kusimama kwenye nafasi yake kuhakikisha inakuwa ni sahihi na kwamba endapo itashindikana kuzingatia ushauri wao waende kwenye vyombo vya sheria.

Kuhusu Katiba mpya, wagombea walisema iliyopo sasa ina mambo mengi yamepitwa na wakati na ipo haja ya kuwa na nyingine ambayo itaendana na wakati wa sasa.

"Katiba ni ya mwaka 1977, na kwa sasa kuna mambo mengi sana, kuna maendeleo yamefikiwa, na Katiba ya sasa ina maeneo mengi sana ambayo kuna mapungufu ambayo kimsingi kila mmoja angependa kuwa na Katiba mpya, kama mshauri wa masuala ya kisheria, nikichaguliwa kuwa rais wa TLS, moja ya ajenda kubwa itakuwa ni kushauri kurudishwa mchakato uliokuwa umeshaanza ili iendane na nyakati za sasa," alisema Nkuba.

Emmanuel Muga, alizungumzia kuhusu Mwabukusi kuenguliwa na baadaye kurejeshwa huku akitahadharisha watu kuacha kuhusisha suala hilo na mambo ya kisiasa.

"Mimi nadhani kwamba tuache siasa na mambo ya dhana kwa sababu sisi ni wanasheria, ndani ya TLS hakuna uonevu, naomba mwelewe kitu kimoja, kuna kamati ambazo tumezi-unda sisi wenyewe, na hii kamati iliyomwengua Mwabukusi, ni kamati ambayo imeundwa na mawakili na sio mtu mwingine ametoka nje. Sisi tunaoenda mahakamani, huwa tunakutana mara nyingi na maamuzi kama haya.

"Lakini ukishakumbana na maamuzi kama hayo, hugeuki ukashika kichwa ukaanza kupiga mateke kwenye mchanga unalalamika, hapana, unafanya uamuzi wa kwenda juu, ukiamini kwamba kile ambacho nimenyimwa huku chini, bila shaka juu nitakipata, kwa hiyo ni aina ya mfumo wa utoaji haki.

Kuhusu wanawake kutoonekana katika kinyang`anyiro cha urais TLS, walisema kwa sasa kuna ushindani mkubwa katika nafasi hiyo, huenda ni chanzo cha wao kuogopa kujitokeza.

"Kutojitokeza kwa wanawake kunachangiwa na siasa za TLS ambazo kuanzia mwaka 2017 zimekuwa za ushindani mkubwa, zinaogopesha baadhi ya watu, kwa sababu hata ukishachaguliwa bado unakuwa umekalia kiti cha moto na ndio maana hata wanaogombea sasa wanaishia mhula mmoja wanaondoka," alisema Muga.

Nkuba alisema anaamini sababu ya wanawake kutojitokeza katika nafasi hiyo ni kwa sababu ya ushindani na ugumu wa nafasi hiyo na kwamba akichaguliwa ataweka sera ya jinsia ambayo itaeleza namna ya kumwezesha mwanamke katika nafasi za uongozi.

Uchaguzi wa viongozi wapya wa TLS unatarajiwa kufanyika Agosti Mosi na tatu, mwaka huu jijini Dodoma.

# 'Wageni marufuku kukusanya madini vito machimboni'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde, amesema katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Juni 30, 2024, Tume ya Madini ilikusanya zaidi ya Sh. bilioni 753. 8 sawa na asilimia 85.45 ya lengo la makusanyo lililopangwa.

Pia, amepiga marufuku wageni wenye leseni kubwa za biashara ya madini (dealer's license) hususan ya vito kwenda machimboni kukusanya.

Alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayotekelezwa na wizara ya hiyo.

"Katika kipindi cha mwaka 2023/2024, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini ilipanga kukusanya jumla ya Sh. bilioni 882.1 kutokana na vyanzo vilivyoainishwa katika Sheria ya Madini Sura ya 123," alisema.

Alisema, vyanzo hivyo ni pamoja na mrabaha, ada ya mwaka ya leseni, ada ya ukaguzi wa madini, ada za kijiolojia, tozo ya huduma ya maabara na malipo ya adhabu mbalimbali.

"Napenda kuwajulisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2023 hadi tarehe 30 Juni 2024, Tume ya Madini ilikusanya jumla ya Sh. 753,815,646,587.13 sawa na asilimia 85.45 ya lengo la makusanyo lililopangwa.

"Makusanyo haya ni sawa na ongezeko la kiasi cha Sh. bilioni 76. 08 ukilinganisha na fedha zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo makusanyo yalikuwa ni Sh. bilioni 677.7 kwa lengo la kukusanya Sh. bilioni 822.01," alisema.

Alisema, kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2023/2024, makusanyo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na kuwapa imani ya kufikia malengo ya kukusanya Sh. bilioni 999.9 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

"Hapo nyuma kidogo, wizara ilikuwa ikikusanya kiasi kidogo cha maduhuli ukilinganisha na sasa. Mathalan, mwaka wa Fedha 2014/2015, wizara ilikuwa na lengo la kukusanya Sh. bilioni 209.9 na kufanikiwa kukusanya Sh. bilioni 168.04.

"Aidha, mwaka wa fedha 2015/2016 lengo la makusanyo lilikuwa ni Sh. bilioni 211.9 na kufanikiwa kukusanya Sh. bilioni 207.9. Hata hivyo, ndani ya kipindi kifupi tunashuhudia ongezeko la makusanyo ya maduhuli yatokanayo na shughuli za uchimbaji wa madini," alisema.

Kadhalika, alisema mabadiliko hayo ni mafanikio makubwa ambayo wadau wote wa sekta hiyo wanatakiwa kujivunia.

Aidha, alikemea vitendo vya udanyanyifu kwenye biashara ya madini pamoja na utoroshaji vinavyofanywa na watu wachache ambao katika vitendo vyao, wanarudisha nyuma malengo ya serikali.

Alisema, wizara itaendelea kuchukua hatua kali kwa wahusika wote watakaobainika wanajihusisha na utoroshaji.

"Nachukua nafasi hii kupiga marufuku kwa wamiliki wa leseni za uchimbaji mdogo wa madini, kuingiza wageni kutoka nje ya nchi kwenye leseni zao bila kuwa na mikataba/makubaliano ya msaada wa kiufundi (Technical Support) yaliyopitishwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alisema kumetokea tabia ya wamiliki wa leseni za uchimbaji mdogo wa madini kuingia makubaliano yasiyo rasmi na wageni kutoka nje ya nchi na kuwaruhusu kufanya kazi katika leseni zao.

"Ikumbukwe kwamba, leseni za uchimbaji mdogo wa madini zinatolewa kwa Watanzania pekee kwa mujibu wa kifungu cha 8 (2) cha Sheria ya Madini, Sura 123.

"Pia nichukue fursa hii kupiga marufuku wageni wenye leseni kubwa za biashara ya madini (dealer's license) hususan wa madini ya vito kwenda machimboni kukusanya madini," alisema.

Alisema kufanya hivyo ni kupora haki ya ajira ya Watanzania ambao kwa mujibu wa Sheria kazi ya kufuata madini machimboni inapaswa kufanywa na Watanzania pekee wenye kumiliki leseni ya 'broker'.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Muda wa kurekebisha viwanja vya kuchezea Ligi Kuu ni sasa

**RATIBA** ya Ligi Kuu Tanzania Bara imetolewa, ambapo Agosti 16, mwaka huu, kinyang'anyiro hicho cha kusaka ufalme wa soka nchini kwa msimu wa 2024/25 kitaanza rasmi.

Timu kwa sasa zipo kwenye maandalizi ya msimu mpya (pre seasons), zilijiandaa na mbio hizo za msimu mzima, ambazo mbali na kusaka ubingwa zitakuwa zikiwania nafasi nne ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Hiyo ni kutokana na viwango vya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Tanzania inaruhusiwa timu nne kucheza michuano ya kimataifa, hivyo zitakazoshika nafasi hizo za juu, zitacheza michuano hiyo, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Hata hivyo, atakayeshika nafasi ya nne anaweza asicheze Shirikisho, kama bingwa wa Kombe la FA hatotokana na timu tatu zinazomaliza nafasi za juu kwenye Ligi Kuu.

Hivyo kuelekea msimu mpya tunaamini pia waamuzi nao watakuwa wanajinoa ili kuchezesha kwa haki mechi hizo ambazo kwa mara ya kwanza baadhi ya michezo itakuwa na Video ya Kumsaidia Mwamuzi, VAR.

Wakati maandalizi hayo yakiendelea kwa kila idara, rai yetu pia ni kuona wamiliki wa viwanja wakiendelea kuviboresha ili viweze kuwafanya wachezaji kuonyesha vipaji vyao halisi.

Lakini pia waelekeza nguvu zao kuviboresha zaidi kwani viwanja bora huvutia mashabiki kwenda kutazama soka na kuwapa burudani ya kutosha wale wanaoangalia kwenye televisheni.

Ikumbukwe pia hakuna watu wanaopata tabu kuangalia mpira kupitia televisheni halafu uwanja unakuwa mbovu, hautamaniki kabisa, hivyo uboreshwaji wa viwanja ni burudani kwa watazamaji wote lakini pia kutaongeza thamani kwenye ligi yetu ambayo inazidi kukua kila uchwao.

Huu sasa ni wakati wa kufanya marekebisho makubwa hasa upande wa nyasi ziwe za kijani na vipimo sahihi, pamoja na maeneo mengine ambayo huwa yanasahaulika sana kama kwenye vyumba vya kuvalia wachezaji na vyooni.

Tulimsikia Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, akisema kuelekea msimu ujao watakuwa wakali sana kuhusu viwanja na akabainisha kama isipowezekana ni bora ligi ichezwe kwenye viwanja vichache kuliko kuipeleka katika viwanja vibovu.

Tuseme tu tunampongeza Karia kwani haiwezekani Ligi ya Tanzania ambayo inashika nafasi ya sita Afrika ichezwe kwenye viwanja vyenye ubora hafifu.

Pamoja na hayo kuna tabia ya wamiliki au mameneja wanatengeneza viwanja vinavyokuwa vizuri wakati ligi inaanza lakini baada ya mechi tatu havitamaniki.

Na hii ni kwa sababu ya kuruhusu mechi nyingi za mashindano ya vikombe, pamoja na timu za mkoa husika kufanya mazoezi katika viwanja hivyo.


Tunashauri mameneja kupiga marufuku viwanja hivyo kutumiwa kwenye mazoezi mara kwa mara, badala yake vitumike katika ligi na michezo mikubwa tu hususan za Ligi Kuu na Ligi za Chanpionship, pia zinaweza kufanya mazoezi kwenye viwanja vingine.

Kuchezwa mechi mbili au tatu, halafu timu zinahama uwanja ni kutowatendea haki mashabiki wa mkoa husika wakiwamo wafanyabiashara, lakini pia kuhama kwa timu mwenyeji kunaipotezea mapato mengi kwa kuwa haiwezi kupata mashabiki wengi uwanjani ikiwa ugenini.

Hasa ikizingatiwa kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu Bara, timu mwenyeji ndiyo inachukuwa mapato yote ya mlangoni katika mechi husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kibu kazidi kuonesha kwa nini wazawa hawaaminiki

Na Adam Fungamwango

**KUNA** wakala mmoja wa wachezaji, aliwahi kuniambia ukimpeleka mchezaji wa Kitanzania nje ya nchi mpaka wamchukue au kumfanyia majaribio ni lazima awe na barua kutoka klabu yake ya mwisho aliyotoka, vinginevyo hawatomruhusu kufanya chochote.

Akasema sababu kubwa klabu nyingi za nje wameshawahi kuingia matatizoni kwa kuwafanyia majaribio wachezaji ambao wana mikataba na klabu wanayotoka.

Akasema baadhi ya klabu zimeshawahi kulipa faini kutokana na hilo, kwani wachezaji walikuwa wakizidanganya kuwa hawakuwa na timu, yaani wapo huru.

Na hilo limekuwa likiwafanya wasiaminike tena kwenye klabu na wakati mwingine kutowaongeza mikataba wanapomaliza ile ya kwanza.

Sakata la Kibu Denis ambalo limeshika chati kwa kiasi cha wiki nzima kwenye vipindi vya michezo, vijiweni, mitaani na mitandao ya kijamii, limenifanya nimkumbuke wakala huyo.

Sitaki kueleza mengi jinsi alivyokuwa mapumzikoni nchini Marekani, halafu wakati wenzake wanataka kwenda nchini Misri yeye akaenda Kigoma na baada ya hapo akatoweka huku kikosi cha Simba kikiwa kwenye maandalizi ya msimu huko Ismailia, Misri. Hakuna aliyejeua amekwenda wapi, hata wasimamizi wake nao walipoulizwa hawakujua yupo wapi, klabu nayo haijui, hali ambayo ilisababisha mtafaruku mkubwa.

Taarifa zikadai kuwa ametorokea Ulaya kusaka malisho, lakini kila mmoja akashangaa uondokaji wake wakati ana mkataba mbichi na Klabu ya Simba, iliyomsajili kwa mbinde.

Baada ya sakata zima, imeelezwa kuwa kumbe alitimkia nchini Norway kwenye Klabu ya Kristiansund BK.

Kwa akili yake alidhani angeweza tu kwenda na kusajili bila klabu yake kufahamu, au kuna kitu alitegemea.

Wengi wanaofahamu mpira wa kisasa hasa wa kulipwa unavyoendeshwa, walijua hata iwe vipi hatocheza mpaka ruhusa rasmi ya klabu yake, labda tu awe hajaingia mkataba.

Ndicho kilichotokea, klabu hiyo imekiri kwamba haikuambiwa ukweli kuhusiana na mchezaji hali iliyosababisha wao kufanya makosa ya kuwasiliana na kumtumia mwaliko mchezaji mwenye mkataba unaozidi miezi sita bila kwanza kuwasiliana na klabu na kupata ruhusa ya kukubaliwa mwaliko huo. Klabu imekiri kukiuka taratibu na Kanuni za FIFA na imeona hatari iliyopo mbele yao.

Habari zinasema Simba iko tayari kumuachia Kibu aondoke, ila inataka kipengele ilichokiweka cha kuuzwa mchezaji huyo kifikiwe, ambacho ni dola za Kimarekani milioni moja, sawa na kiasi cha Sh. bilioni 2.7 za Kitanzania, wakiwa hawataki kusikia kuhusu majaribio kwa kuwa kuna kukosa na kupata, ikitokea akakosa na kurudi itakuwa imetoa mwanya kwa wachezaji wao wengine kuondoka kihuni.

Ina maana hapa Kibu amekwama. Kama ni akili yake mwenyewe au kuna waliokuwa wanamshawishi, basi hawakumshauri vizuri. Hatogusa mpira mpaka Simba waruhusu. Hili nadhani litakuwa fundisho kwa wachezaji wengine hasa wa Kitanzania.

Huku ndiko tunaona hata usajili wa timu mbili, huwezi kuona mchezaji yeyote wa kigeni kutoka nje kasaini timu mbili, utata kwenye usajili wake, au asajili timu halafu haendi kuitumikia, au anatimka nje.

Hili limefanywa pia na Lameck Lawi ambaye amechukua pesa za Simba, lakini kwa sasa ametimkia Ubelgiji. Kwa sasa Simba na Coastal ambazo ziliwashiana moto kuhusu suala hili, wameamua kukaa ili kulizungumza kama walivyoamriwa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji.

Nadhani tabia hii imewafanya wachezaji wa Kibongo wasiaminike, na hii itawaponza zaidi huko mbele ya safari kwani klabu zitakuwa zikiogopa kuwasajili, badala yake kwenda nje kusajili wachezaji ambao wanafahamu maana ya mikataba na kuiheshimu.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa achangisha mil. 900/- ujenzi wa kanisa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameendesha harambee na kuchangisha Sh. milioni 928.67 za ujenzi wa kanisa kuu tarajiwa la Mt. Andrea Kagwa la Jimbo Katoliki la Lindi.

Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 464.3 ni fedha taslimu (nyingine zimeshawekwa benki) na Sh. milioni 464.37 ni ahadi. Awamu ya kwanza ya ujenzi huo inatarajiwa kugharimu Sh. milioni 700.

Akizungumza na waumini na wadau mbalimbali waliohudhuria harambee iliyofanyika mjini Ruangwa juzi, Waziri Mkuu aliwataka waliotoa ahadi wazikamilishe mapema ili kazi ya ujenzi isikwame.

"Ninawashukuru sana wote mliofika na wote waliochangia ujenzi wa kanisa tarajiwa. Ninawaomba walioahidi, wakamilishe ahadi zao mapema ili kazi ianze kwa kuwa ramani ipo, mafundi wapo tayari, wasimamizi wa ujenzi wapo," alisisitiza.

Waziri Mkuu alisema uamuzi wa Baba Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi, Mhashamu Askofu Wolfgang Pisa, kuanza ujenzi wa kanisa kuu la jimbo hilo, ni utekelezaji maono aliyokuwa nayo tangu aliposimikwa kuongoza jimbo hilo Juni 2022.

"Mhashamu Baba Askofu Pisa ameanza kutekeleza maono yake kupitia kaulimbiu ya 'Ninaona Kiu' aliyoitangaza tarehe 26 Juni 2022 wakati akisimikwa kuwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi.

"Ninaomba wanaLindi tumpe ushirikiano kwa sababu maono yake ni endelevu. Ninawasihi tumpe ushirikiano ili aweze kutimiza hayo maono," alisema.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwasihi wazazi na walezi wawe karibu na watoto wao na wafuatilie hatua za ukuaji wao ili baadaye wawe raia wema.

Awali akisoma risala kuhusu mradi wa ujenzi wa kanisa tarajiwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Fortunatus Machibya alisema harambee hiyo imelenga kukusanya Sh. milioni 900 ambapo kati ya hizo, Sh. milioni 700 ni za ujenzi na Sh. milioni 200 ni za maandalizi ya Jubilei ya Miaka 25 ya upadrisho wa Askofu Pisa na miaka 50 ya Askofu Mstaafu wa Jimbo la Lindi, Mhashamu Askofu Bruno Ngonyani.

Alisema ujenzi wa kanisa hilo unahitajika kukamilika haraka kwa sababu wakati Jimbo Katoliki la Lindi linaanzishwa mwaka 1986, kanisa lililopo lilipewa tu hadhi na hapakuwa na kanisa jipya.

"Kanisa lililopo ni dogo, ni la zamani na uwezo wake ni kuchukua watu 600 wakati matukio ya kikanisa huwa yanaleta watu zaidi ya 1,000. Tumeamua kujenga kanisa jipya lenye uwezo wa kuchukua watu 2,000 kwa wakati mmoja badala ya kufanya ukarabati na kupoteza fedha.

"Hili tutalijenga kwa awamu kwa miaka mitano, na hadi likamilike tunatarajia kutumia Sh. bilioni 6.6," alisema.

Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na Askofu wa Jimbo Katoliki la Mtwara, Mhashamu Titus Mdoe, Mkuu wa Mkoa wa



Mwenyekiti wa Taifa wa ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, akiwa kwenye mkutano wa hadhara katika viwanja vya Jadida Wete, Pemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yaja na mbinu kukabili uhaba wa ajira kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo umesema utamaliza tatizo la ajira nchini ili kupunguza umaskini, kuboresha maisha na kukuza maendeleo ya kiuchumi ukipewa madaraka na wananchi.

Umesema utachukua hatua madhubuti za kupunguza matumizi ya anasa zinazofanywa na serikali, kuweka vivutio vya kikodi na kuondoa masharti magumu kwa vijana wanaoanza biashara ndogo na kufuta sheria zote kandamizi.

Msimamo huo ulielezwa mwishoni mwa wiki na viongozi wakuu wa ACT Wazalendo wakiwa katika majimbo ya Singida Mjini (Singida), Muhambwe (Kigoma), Rorya (Mara) na Namtumbo (Ruvuma), wakiendelea na awamu ya kwanza ya ziara ya kuyafikia majimbo yote 214 ya Tanzania Bara.

Kiongozi wa Chama, Dorothy Manka Semu, akiwa Jimbo la Singida Mjini, alisema kuwa ili kuleta heshima na utu, lazima vijana wapatiwe fursa za ajira na shughuli za uhakika za kujipatia kipato.

Alisema ACT Wazalendo imejizatiti kupanua soko la ajira na kuhakikisha kila Mtanzania ana shughuli ya uhakika wa kujipatia kipato.

"Wazee wetu enzi za TANU walitambia kazi ni kipimo cha utu, lakini CCM imeshindwa kuendesha uchumi unaozalisha ajira na kazi zenye staha. Utu sasa unapimwaje?

"Serikali haitaki kuajiri lakini inafanya matumizi ya anasa kwa kujiongea posho, safari za nje, sherehe na kununua magari ya kifahari," alilalama.

Dorothy alisema kuwa ACT-Wazalendo itapunguza matumizi ya anasa ya serikali ili kutumia fedha hizo kutoa ajira mpya kwa vijana nchini.

Alitolea mfano kupunguza ununuzi wa magari ya kifahari ya viongozi, kudhibiti ubadhirifu wa fedha za umma na kutaifisha mali zote za watu waliokutwa na ubadhirifu. Dorothy alisema ACT-Wazalendo itafuta sherehe zisizo za lazima kama vile mbio za Mwenge wa Uhuru na dhifa zingine.

Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchinjita, akiwa jimboni Namtumbo, alisema serikali ya ACT-Wazalendo itahakikisha vijana wanaohitimu wanapata ajira kulingana na taaluma zao.

Alisema msisitizo utawekwa hasa katika sekta nyeti zenye upungufu mkubwa wa wataalamu kama vile elimu, afya na kilimo, akilalama kuwa vijana wengi wako mtaani hawajaajiriwa.

"Tatizo la ajira kwa vijana wahitimu limetengenezwa na CCM kwa kushindwa kuwaajiri vijana hao. Tuna mahitaji makubwa kwenye sekta ya afya, elimu na kilimo.

"ACT-Wazalendo itahakikisha inatoa ajira mpya 65,000 kwa sekta ya elimu ajira, wahudumu wa afya 21,000 kwa miaka mitano mfululizo," alisema Mchinjita.

Ado Shaibu, Katibu Mkuu wa chama hicho, alisema ACT-Wazalendo itaweka mazingira mazuri ya kibiashara, kilimo na shughuli zingine za wananchi.

"Mazingira ya sasa ya kiuzalishaji na biashara yanakandamiza vijana walio wengi. ACT-Wazalendo itaondoa mfumo wa kulipia kodi kabla ya kuanza biashara, itawapa uhuru wananchi na kuondoa urasimu katika kuanzisha biashara," alisema. Suala lingine alilogusia ni kufungamanisha sekta ya uzalishaji wa ndani na utekelezaji miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli ya kisasa na uchimbaji chuma ili kuongeza ajira.

Alisema mahitaji ya nchi na uzalishaji wa viwanda pamoja na kilimo yanaonesha ni muhimu kufungamanisha sekta hizo kama njia za kuzalishia ajira mpya zaidi.

Msisitizo kuhusu dhamira ya ACT- Wazalendo kutengeneza uchumi unaozalisha ajira ulitolewa pia na Kiongozi mstaafu wa chama hicho, Zitto Kabwe, ambaye akiwa Jimbo la Muhambwe, mkoani Kigoma juzi, alisema utawala wa CCM umeshindwa kuzalishia ajira za uhakika zenye staha kwa miaka 60 tangu uhuru wa nchi.


"Vijana wa Tanzania wanataka ajira, ajira zenye staha, watawala kwa miaka zaidi ya 60 sasa wameshindwa. ACT Wazalendo inayo mikakati ya kujenga uchumi unaokua kwa kasi na kuzalishia ajira nyingi na zenye staha," alisema.

Alitaja hatua hizo ni pamoja na kuongeza bajeti ya kilimo kufikia asilimia 20 ya bajeti ya serikali kuu ili kuhakikisha kilimo kinakua kwa wastani wa asilimia 10 kwa mwaka.

Hatua nyingine, Zitto alitaja ni kutoa vivutio maalum vya kikodi kwa kampuni binafsi zitakazotoa nafasi ya ajira kwa vijana waliohitimu elimu ya vyuo mbalimbali.

Jana viongozi wa ACT-Wazalendo waliendelea na ziara katika majimbo ya Kasulu Vijijini (Kigoma), Butiama (Mara), Hanang' (Manyara) na Tunduru Kaskazini (Mkoa wa Kichama Selous).

KABWELA — Na Fadhili Mohammed






Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Lugha, Asia na Afrika ambaye ni Naibu Mhariri Mkuu wa CGTN, An Xiaoyu, akizungumza katika kongamano hilo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: CGM**

# China inavyofungua milango ya fursa barani Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

KONGAMANO la Kunufaika Pamoja na Fursa za Mageuzi ya China la Shirika Kuu la Utangazaji la China (CMG) limefanyika Julai 22, jijini Dar es Salaam ikiwa ni shughuli ya kwanza ya uenezi kuhusu Mkutano wa Tatu wa Wajumbe wote wa Kamati Kuu ya 20 ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) iliyoandaliwa na CMG barani Afrika.

Watu zaidi ya 40 kutoka vyombo vya habari vikubwa, taasisi za washauri bingwa na wafanyakazi wa ubalozi wa China nchini Tanzania walihudhuria kongamano hilo. Wajumbe hao walisikiliza hotuba ya Rais Xi Jinping, ambaye ni kiongozi mkuu wa CPC akiongoza mageuzi ya kina ya "China katika Zama Mpya".

Mkuu wa CMG, Shen Haixiong, aliwaambia washiriki wa kongomano hilo kuwa amefurahishwa na wageni hao kufuatilia Mkutano wa Tatu wa Wajumbe Wote wa Kamati Kuu ya 20 ya CPC, wakisifu mafanikio ya mageuzi na ufunguaji mlango wa China na kuwa na matarajio makubwa na fursa zitakazoletwa na mageuzi mapya ya China kwa Afrika.

Mkurugenzi wa Idara ya Asia na Afrika ya CMG, An Xiaoyu, aliwaambia wajumbe maana ya historia ya Mkutano wa tatu wa Wajumbe Wote wa Kamati Kuu ya 20 ya CPC, akisema azimio lililopitishwa na Mkutano huo limeonesha sifa ya maendeleo ya kisasa ya China, na kwa kupitia kuhimiza maendeleo ya hali ya juu na ufunguaji mlango wa kina, China italeta uhakika muhimu kwa dunia iliyojaa sintofahamu na kuunda fursa zaidi za maendeleo.

Akitoa maoni kuhusu fursa mpya ambazo China italeta kupitia kuimarisha mageuzi katika zama mpya, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Umoja wa Vijana wa Afrika na mchumi maarufu wa Afrika, Francis Matambalya alisema nchi za Afrika zinahitaji kuboresha uwezo wa utawala wa nchi, na uzoefu wa China una thamani kubwa.

Alisema uhusiano kati ya China na Afrika umejengwa katika msingi imara wa kuheshimiana na ushirikiano wa kusaidiana na kunufaishana, jambo ambalo ni tofauti kabisa na nchi za Magharibi.

"Katika zama mpya, kama nchi za Afrika zinaweza kutumia zaidi fursa zinazoletwa na mageuzi ya China au la, hii itakuwa na athari kubwa kwa mustakabali wao," alisema.

Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe Beatrice Bandawe alisema amefurahi kuona kuwa chini ya uongozi wa Rais Xi, China inachukua hatua za kivitendo kusaidia maendeleo ya kijani barani Afrika, Tanzania na Afrika zinaichukulia China kama mshirika muhimu wa ushirikiano anayetegemewa.

Na kuwa China siku zote imekuwa mbele kuwekeza katika nchi nyingine zinazoendelea, na Tanzania na nchi nyingine za Afrika zinatarajia kupanua zaidi ushirikiano na China. Mwenyekiti wa Kituo cha Utafiti wa Kiswahili cha Mwalimu Nyerere, Profesa Aldin Kai Mutembei, alisema mafanikio ya kiuchumi ya China ni ushahidi bora wa mafanikio ya mageuzi na kufungua mlango.

"China imeithibitishia dunia mafanikio ya mfumo wa ujamaa wenye umaalum wa China kupitia maendeleo yake ya kijamii na kiuchumi," alisema.

Alisisitiza kuwa ujenzi wa mfumo wa demokrasia na mtindo wa usimamizi wa jamii pia ni mfano wa kuigwa kwa nchi za Afrika.

Mhadhiri wa Uchumi na Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa China katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Humphrey Moshi, alisema utaratibu wa ushirikiano kati ya China na nchi zinazoendelea ni chachu muhimu ya kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi hizo.

Tofauti na nchi za Magharibi, China inaheshimu matakwa ya kila nchi ya Afrika na ina vipaumbele tofauti katika ushirikiano na nchi tofauti.

Ushirikiano kati ya China na Afrika umejengwa kwenye mazungumzo na unaonyesha sifa za kuheshimiana na usawa.

Alitoa wito kwa China na Afrika kuanzisha mfumo wa kufunga mahesabu za kifedha na kibiashara kwa kutumia sarafu ya China (RMB), na pia anatumaini kuwa nchi hiyo itahimiza maendeleo ya sekta ya nishati mpya barani Afrika.

Mkuu wa Kituo cha Televisheni cha Star TV cha Tanzania, Steve Diallo, alisema China ni mshirika mkuu wa biashara wa Afrika, na mtindo wa maendeleo ya uchumi wa nchi hiyo kupitia mageuzi na ufunguaji mlango ni mfano wa kuigwa kwa Tanzania.

Kwa sasa, ushirikiano kati ya China na Tanzania umejikita zaidi katika miundombinu, kilimo, madini na biashara, na anatarajia kuwa nchi hizo mbili zinaweza kuimarisha ushirikiano na mawasiliano kati ya vyombo vya habari katika siku zijazo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Africa Media Group, Augustino Mganga, alipongeza mafanikio ya Mkutano wa Tatu wa Wajumbe wote wa Kamati Kuu ya 20 ya CPC.

"Nimesoma baadhi ya vitabu kuhusu fikra za Rais Xi Jinping, na nakubaliana sana na pendekezo lake la kujenga jumuiya ya binadamu yenye mustakabali wa pamoja. Mkakati wa utawala wa nchi wa Rais Xi Jinping unaielekeza China kuboresha sifa ya uchumi wake kupitia uvumbuzi wa sayansi na teknolojia, na pia kuwezesha bidhaa za teknolojia ya juu na huduma za China kunufaisha nchi nyingine.

Chini ya uongozi wa Rais Xi, mawasiliano ya kitamaduni yanayoimarika kati ya China na Tanzania yamewawezesha watu wa Tanzania kunufaika na maendeleo ya kisasa ya China," alisema.

## Akutwa amejinyonga hadi kufa ofisi ya kijiji

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MKAZI wa Kijiji cha Kiyaula, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Bahati Ngailo (20), amekutwa amejinyonga hadi kufa kwenye ofisi ya kijiji kwa kutumia fulana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga, alisema tukio hilo limetokea Julai 24, mwaka huu majira ya saa 2:06 asubuhi kwenye chumba cha mahabusu ya ofisi ya kijiji.

Kamanda Banga alisema Ngailo alifungiwa katika ofisi hiyo baada ya kutuhumiwa kuvunja nyumba na kuiba Sh. 600,000, mali ya Martine Ngailo (67).

Kamanda alisema kutokana na tukio hilo wanawashikilia watuhumiwa wawili ambao ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Adamu Kiswaga (33) na Erick Mligo (25), askari mgambo kwa uzembe wa kutotoa taarifa na kutomfikisha mtuhumiwa kituo cha polisi kilicho karibu.

"Natoa wito kwa viongozi wa serikali ikiwamo watendaji wa vijiji na kata wanapokuwa wanashughulikia kesi ambazo zinamwelekeo wa jinai watoe taarifa kwenye vituo vya polisi na sio kulaza watu kwenye mahabusu za vijiji ambapo mwisho wa siku uzembe wao unapelekea mtu kutenda tukio la namna hiyo," alionya Kamanda Banga.

## Wamlalamikia Rais Samia kupunjwa fidia mradi SGR

**Na Kulwa Mzee**

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Guluka Kwalala, Pugu waliopisha mradi wa Reli ya SGR, wamemwandikia barua Rais Samia Suluhu Hassan wakilalamikia kulipwa kiasi kidogo tofauti na malipo halisi yaliyopo kwenye tathmini.

Wananchi hao walizungumzia mapunjo yao jana wakionyesha jitihada wanazofanya ili kupata fedha zao, bila mafanikio.

Akizungumzia tukio hilo, Damali Mazubesi alisema ni miongoni mwa wananchi wa Mtaa wa Galuka Kwalala Km18, waliopisha mradi walifanyiwa tathmini mwaka 2019.

"Malipo yangu nilioneshwa jumla yalikuwa Sh 191,751,875, lakini nilikuja kulipwa Sh. 165,913,695 na hakukuwa na mchanganuo kuonyesha kipi kililipwa kiasi gani, hesabu zikalipwa kwa jumla," alisema.

Alisema fedha alizopunjwa ni Sh. 25,913,695 na aliandika barua za malalamiko sehemu mbalimbali ikiwamo Shirika la Reli, lakini hadi sasa hajalipwa.

Alisema eneo lake lilikuwa kubwa lenye nyumba kubwa, nyumba ndogo, flemu za biashara nne, uzio, miti na mazao mbalimbali, lakini katika malipo aliyolipwa hakuna ufafanuzi kiasi gani kalipwa kwa ajili ya kitu gani.

Mwananchi mwingine aliyepunjwa fidia, Boaz Mabuga alisema eneo lake lilikuwa na ukubwa wa mita za mraba 1071 na malipo yake halisi yalikuwa Sh. 72,205,000, lakini alilipwa Sh 63,000,000 ikiwa pungufu ya Shilingi milioni tisa.

"Nililalamika kwa kuandika barua lakini nilivyofatilia nilibaini eneo lilipunguzwa ukubwa, fedha walizolipa za 'Square' mita 735 badala ya 1071."

Ally Hamad alisema malipo halisi yalikuwa Sh. 79,900,000, lakini amelipwa Sh. 66,400,000.

"Muda umeshakuwa mrefu hakuna kinachoendelea, kulikuwa na shimo la choo ambalo thamani yake ilikuwa Sh milioni 3.5 lakini kwenye malipo sikulipwa," alisema Hamad.

Alipoulizwa Mtendaji wa Kata hiyo, Rose Zuberi alisema alihamia katika eneo hilo mwaka 2021 mradi unaolalamikiwa ulikuwa umeshapita.

"Hapa ofisini naona wananchi wanakuja mmoja mmoja wakizungumzia mradi wa reli na mapunjo, tunawaelekeza waandike barua za malalamiko, wengine wanaandika, lakini hakuna aliyelipwa madai wanayolalamikia," alisema.

**TANGAZO**

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNE 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Jun-24 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Mar-24 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,898 | 4,627 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,382 | 21,738 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 39,032 | 42,067 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,548 | 5,238 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 330 | 281 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 19,927 | 92,783 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 143,169 | 133,251 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 14,485 | 13,991 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,519 | 1,519 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,630 | 2,508 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **245,920** | **318,003** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 19,049 | 30,209 |
| 18 | Amana za Wateja | 167,823 | 158,171 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,242 | 3,753 |
| 28 | Madeni | 6,423 | 117,256 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **197,536** | **309,390** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **48,384** | **8,613** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 159,426 | 139,306 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,233 | 200 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (115,183) | (133,915) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 219 | (210) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 688 | 3,233 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **48,384** | **8,613** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 17,452 | 9,936 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,233 | 6,364 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,253 | 5,155 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 19.67% | 2.71% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.22% | 4.60% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.42% | 73.47% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58.22% | 41.90% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.23% | 85.96% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.80% | 9.16% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -22.67% | 5.76% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNE 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(133,683)** | **-** | **-** | **3,233** | **8,856** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 219 | - | - | - | **219** |
| Hisa za upendeleo | 20,120 | - | - | - | - | - | **20,120** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (688) | 688 | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | 19,205 | - | - | - | **19,205** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **159,426** | **-** | **(114,964)** | **688** | **-** | **3,233** | **48,384** |
| | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Mwaka Uliopita** | - | - | - | - | - | - | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(120,704)** | **-** | **-** | **3,018** | **5,268** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (12,979) | - | - | - | **(12,979)** |
| Hisa za upendeleo | 16,352 | - | - | - | - | - | **16,352** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | 215 | **215** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(133,683)** | **-** | **-** | **3,233** | **8,856** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNE 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-24 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 8,834 | 10,377 | 19,563 | 20,660 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,097) | (4,787) | (7,005) | (9,707) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,737** | **5,590** | **12,558** | **10,953** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 238 | 544 | 516 | 553 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,472) | (300) | (1,613) | (300) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **2,867** | **1,534** | **4,079** | **2,792** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,891 | 408 | 2,433 | 927 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 400 | 377 | 741 | 675 |
| | 6.3 Gawio | 40 | - | 40 | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 536 | 749 | 864 | 1,190 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,889)** | **(7,887)** | **(15,216)** | **(15,598)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,958) | (2,865) | (5,826) | (2,865) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,930) | (5,022) | (9,390) | (12,733) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **482** | **(520)** | **324** | **(1,599)** |
| **9** | Tengo la Kodi ya Mapato | (53) | (59) | (105) | (117) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **430** | **(579)** | **219** | **(1,717)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **430** | **(579)** | **219** | **(1,717)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 170 | 172 | 170 | 172 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 17% | -24% | 2% | -17% |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.68% | -0.67% | 0.23% | -1.03% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6.03% | -8.74% | 1.54% | -12.97% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 82.14% | 110.72% | 91.46% | 113.48% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.46% | 8.40% | 10.68% | 8.23% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNE 2024

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-24 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-24 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 482 | (158) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,472 | 698 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (12,815) | (2,252) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,509) | 15,801 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 3,034 | (744) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 489 | (992) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 72,362 | 6,663 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (53) | (53) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **63,462** | **18,963** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | 36 | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (887) | (376) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(851)** | **(376)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (110,833) | 2,737 |
| | Mengineyo (bainisha) | 20,120 | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(90,713)** | **2,737** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (28,101) | 21,326 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 52,929 | 31,603 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **24,827** | **52,929** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 29-Jul-24 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 29-Jul-24 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 29-Jul-24 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 29-Jul-24 |
| 2 Mkurugenzi | B. Jonker | | 29-Jul-24 |



BancABC part of atlasmara

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| | | | |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| | | | |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| | | | |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order – internal same customer ( set up fee – once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order – internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order – Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges – Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges – Financial Institution – small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local – TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local – EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

| AGENCY BANKING FEE | |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Bill payment | Free |

**Withdrawal Fees**

| Transaction tiers | BancABC Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 0-999 | N/A | – | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |


# Wananchi walia ulipuaji miamba kuathiri makazi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa vijiji 14 vinavyozunguka Mgodi wa Barrick Bulyanhulu uliopo Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamesema ulipuaji miamba mara kwa mara mgodini humo, unasababisha nyumba zao kupata nyufa na vumbi hali inayowafanya wawe na hofu ya kupata magonjwa kama kifua kikuu.

Wananchi hao walibainisha hayo juzi katika kikao cha kukusanya maoni ya Mpango kazi wa Kitaifa wa Tume wa Haki za Binadamu na Biashara uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Kakola-Bulyanhulu na kuendeshwa na Makamu Mwenyekiti wa tume hiyo, Mohamed Hamisi pamoja na viongozi wa vijiji hivyo.

Mkazi wa Kitongoji cha Roma, Joffrey Mang'ombe, alisema ulipuaji wa miamba mgodini umekuwa ukisababisha nyumba zao kupata mipasuko na kuingia gharama ya marekebisho mara kwa mara na hivi karibu ulitokea ulipuko mkubwa na kusababisha choo kuanguka.

Joyce Mashauri alisema wakati mwingine wanadai ni tetemeko linakuwa limepita na huku vumbi kali inatimuka kutoka mgodini na kuingia kwenye makazi yao na kusababisha kila kitu ndani ya nyumba kubadilika rangi na athari za kiafya ikiwa ni pamoja na mafua na vikohozi vya mara kwa mara.

Akijibu malalamiko hayo, Meneja Mahusiano na Mazingira wa Barrick Bulyanhulu, Agapiti Paul, alisema sio kweli ulipuaji unaofanywa mgodini umeathiri makazi ya wananchi bali wengi wamejenga makazi yao kwa tofauli za tope ndio sababu zinaleta nyufa na vumbi linalotokana na magari kupita barabarani.

Alisema suala la vumbi linakwenda kuisha baada ya kuanza kwa ujenzi wa barabara ya lami kilometa 73 kutoka lango la mgodi mpaka Kahama.

Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Hamisi alisema malalamiko yote yaliyowasilishwa yatayafikisha kwenye mamlaka sehemu husika, ili kuangalia namna ya kuyatafutia ufumbuzi wake wa haraka kwani amebaini kuwepo kwa baadhi ya malalamiko tangu kuanza ujenzi wa mgodi huo mpaka sasa hayajatatuliwa.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, akipima afya yake kwenye kambi ya matibabu ya afya code clinic mkoani humo, iliyoratibiwa na kampuni ya Jambo Group na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa huo kwa ajili ya kutoa matibabu bure kwa wananchi, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Sengerema kukabidhiwa shule mpya 11 za sekondari

**Elizabeth Seleman** SENGEREMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza inatarajia kupokea shule mpya 11 za sekondari, zinazoendelea kujengwa zikitarajiwa kuanza kutumiwa na wanafunzi ifikapo Januari, 2025.

Akikagua maendeleo ya ujenzi wa shule hizo pamoja na ukarabati wa shule za msingi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Binuru Shekidele, alisema kukamilika kwa shule hizo kutasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani, utoro pamoja na kutembea umbali mrefu. Shule hizo mpya zinazotarajiwa kukabidhiwa ni pamoja na Igulumuki, Isole, Chamabanda, Busulwagili, Kagunga, Nyitundu, Balatogwa, Kabusuri pamoja na Ilekanilo ambazo zinajengwa kwa fedha za serikali kuu na baadhi kwa kushiriana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ambako kukamilika kwake kutaifanya Sengerema kuwa na shule 46 za sekondari. Akiongea na walimu wa sekondari ya Ibisabageni Mkurugenzi huyo, aliwataka walimu shuleni hapo kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuinua kiwango cha taaluma katika halmashauri hiyo.

Aidha, aliwaahidi watumishi wakiwamo walimu wenye sifa na vigezo vya kupanda madaraja watapanda bila kuwepo na upendeleo wowote.

Nipashe
Spotika



10 - BORA YA USAJILI WA MAJIRA YA JOTO HADI SASA UK. 12



Diogo Costa

# MAKIPA WA4 WA KUMRITHI EDERSON MANCHESTER CITY

**MANCHESTER, England**

EDERSON ndiye mlinda mlango ambaye amekuwa kipa bora tangu uhamisho wake wa fedha nyingi kwenda Manchester City mnamo 2017.

Mbrazil huyo, ambaye hakujulikana sana wakati huo, amelinda wavu kwa uhakika, lakini ni kile alichompa Pep Guardiola na mpira miguuni mwake ambacho kimeonekana kuwa muhimu zaidi.

Lakini City sasa wanajiandaa kutokuwapo kwake. Ederson amekuwa akihusishwa sana na kujiunga na Ligi Kuu ya Saudia, msimu huu wa majira ya joto.

Hata Guardiola amekiri kwamba mustakabali wake katika Uwanja wa Etihad haujulikani, huku viatu vya ukubwa vya mchezaji huyo wa miaka 30, vinahitaji kujazwa iwapo ataondoka.

Hapa kuna makipa wengi wenye vipaji kote Ulaya, lakini ni nyota gani wanaweza kuchukua nafasi ya Ederson?

**Unai Simon**

Yeyote asiye na uhakika na uwezo wa Unai Simon, anahitaji tu kuangalia Euro 2024. Kipa huyo wa Hispania alikuwa muhimu kwa 'La Roja' kwani walitawazwa mabingwa wa bara.

Kwenye LaLiga msimu uliopita, mlinda mlango huyo wa muda mrefu wa Athletic Club aliongoza katika orodha ya kuokoa asilimia 74.4.

Lakini Simon vile vile ana kipaji linapokuja suala la usambazaji wa mpira. Huwezi kuichezea Hispania ikiwa huna uwezo. Kwa sasa ana umri wa miaka 27, anaweza kuwa mrithi mzuri wa Ederson.

**Justin Bijlow**

Kocha mpya wa Liverpool, Arne Slot, anajua jambo moja au mawili kuhusu Justin Bijlow. Kocha huyo wa zamani wa Feyenoord alimsaidia mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uholanzi kuwa golikipa mwenye uwezo wa kuokoa na kuwa na matarajio mazuri nje ya eneo lake la hatari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amezivutia Manchester United na Arsenal hapo awali na ni wazi kuona kwa nini. Mtindo wake unaendana na timu zinazotaka kucheza kwa safu ya juu na zile ambazo kwa ujumla zinatumia mbinu inayotegemea umiliki.

Bijlow aliorodheshwa katika asilimia nne bora ya makipa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023/24 kwa kujilinda nje ya eneo lake la hatari (3) na pasi alizojaribu (41.5) kwa kila mechi.

**Diogo Costa**

Diogo Costa ni mlinda mlango ambaye amekuwa akifikiriwa na klabu nyingi baada ya kufanya vema akiwa na Porto na Ureno.

Kwa mchezo wa mwisho, aliokoa penalti tatu katika mikwaju ya Euro 2024 dhidi ya Slovenia, ambayo kabla yake pia alimnyima Benjamin Sesko kufunga katika muda wa ziada.

Kipa huyo chipukizi ambaye atafikisha umri wa miaka 25 Septemba, mwaka huu, amepitia mazingira yake na anatarajiwa kuhamia kwingineko kwa fedha nyingi, huku Manchester City ikiwa moja ya klabu chache ambazo zinaweza kumudu bei yake ya ajabu. Costa inaweza kugharimu karibu pauni milioni 60 msimu huu wa majira ya joto.

City wanajua faida za kuweka imani katika Ligi Kuu, Ederson akiwa mmoja wa nyota wengi waliowang'oa kutoka daraja la juu la Ureno. Uwezo wa Costa wa kupiga pasi, mbinu makini na kupiga shuti bora kunamfanya kuwa mgombea mkuu kuchukua nafasi ya Mbrazili huyo.

**Stefan Ortega**

Kwa nini usajili wa kipa mpya wakati una mbadala mzuri nyumbani? Hilo linaweza kuwa ndilo jambo ambalo City wanafikiria huku kukiwa na uvumi juu ya kuondoka kwa Ederson, wakati Stefan Ortega akiwa amejaza viatu vyake mara kwa mara katika misimu ya hivi majuzi. Yeye mara chache huweka mguu vibaya pindi anakabidhiwa glavu.

Kikosi cha ajabu cha Mjerumani huyo dhidi ya Son Heung-min mwishoni mwa msimu uliopita - kitu ambacho huenda kilishinda City taji la ligi kinaangazia jinsi anavyoweza kuwa kwenye hatua kubwa, hata kama makosa yake katika fainali ya Kombe la FA, wiki kadhaa baadaye imeonekana gharama kubwa.

Guardiola ni wazi anaamini sana uwezo wa Ortega na anaweza kuridhika na kumpandisha namba moja, ingawa ingehitaji kusajili mchezaji mpya namba mbili. Iwapo yuko tayari kuanza wiki moja baada ya nyingine na nje ya wiki katika msimu mzima kwa mabingwa bado haijajulikana.

## ISIKUPITE

KUELEKEA Tuzo ya Ballon d'Or 2024, mshindi mara nane wa tuzo hiyo, Lionel Messi, akiwa na Inter Miami na Argentina, katika michezo 39 aliyocheza amefunga mabao 28 huku akitoa pasi za mwisho 17 na taji pekee alilobeba msimu huu ni Kombe la Copa America.



## Extra Time

# 10 - BORA YA USAJILI WA MAJIRA YA JOTO HADI SASA



**LONDON, England**

INGAWA Euro 2024 na Copa America zimetawala vichwa vya habari vya soka kwa sehemu kubwa ya majira ya joto hadi sasa, bado kumekuwa na uhamisho mwingi ambao umeweza kuwafanya mashabiki wa soka kufurahishwa pia.

Kuanzia Manchester United hatimaye kuonesha umahiri sokoni, hadi Real Madrid kumsajili mwanasoka bora wa dunia, mashabiki wameona uhamisho mwingi wa kufurahisha ukifanywa.

Hawa ndio wachezaji wetu 10 bora waliosajiliwa msimu huu wa kiangazi hadi sasa...

**10. Daichi Kamada kwenda Crystal Palace (Ada: Huru)**

Crystal Palace walinufaika katika hali ya kutoelewana kati ya Daichi Kamada na Lazio msimu huu wa majira ya joto, na kumnyakua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Japan bila malipo baada ya mazungumzo kuvunjika na timu hiyo ya Serie A.

Ingawa si kipaji cha kuvutia machoni kama Michael Olise anayeondoka, Kamada hakika ni nyongeza nzuri kwa safu ya ushambuliaji ya Palace, na mchezaji huyo hapo awali alicheza soka bora zaidi maishani mwake chini ya Oliver Glasner kule Eintracht Frankfurt.

**9. Archie Gray kwenda Tottenham Hotspur (Ada: Pauni Mil. 30)**

Kwa kocha yeyote mahiri anafahamu kikamilifu kwamba Archie Gray ni mmoja wapo wa vijana wanaotarajiwa kusisimua katika mchezo huo.

Akiwa amekamilisha msimu mzima wa kwanza wenye mafanikio katika soka la kulipwa akiwa na klabu ya utotoni ya Leeds United mnamo 2023/24, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alijipatia fedha nyingi kwenda kwa wababe wa Ligi Kuu England, Tottenham Hotspur msimu huu.

Uwezo wake wa kucheza beki wa kulia na kiungo wa kati utakuwa muhimu sana kwa kocha Ange Postecoglou.

**8. Alvaro Morata kwenda AC Milan (Ada: Pauni Milioni 10.9)**

Pauni milioni 10.9 kwa mshambuliaji ambaye ni nahodha wa taifa lake hadi kutwaa ubingwa wa Euro 2024 na kufunga mabao 21 katika michuano yote msimu wa 2023/24? Ndio, hiyo ni biashara.

Juu ya kiwango kizuri cha Morata kwa Atletico Madrid na Hispania, fowadi huyo pia analeta uzoefu wake Serie A kutoka kwa klabu ya zamani ya Juventus hadi AC Milan, na uwezo wa kuziba pengo la Olivier Giroud katika kitengo cha ushambuliaji cha timu hiyo.

**7. Savio kwenda Manchester City (Ada: Pauni Milioni 30.8)**

Kiufundi, Manchester City walilipa klabu ya Troyes pauni milioni 30.8 kwa Savio.

Kwa kweli, kwa sababu ya muundo wa timu ni kama walijilipa pauni milioni 30.8 kwa Savio.

Bila kujali hali mbaya ya kifedha ya uhamisho huu, Man City walionekana kusajili mchezaji mmoja. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alikuwa anaitumikia Girona, klabu nyingine ya CFG, katika msimu mzima wa 2023/24, akiwaongoza kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza katika historia yao na mchango wake wa mabao 19 kwenye La Liga.

**6. Joshua Zirkzee kwenda Man United (Ada: Pauni Mil. 35)**

Mshambuliaji anayelinganishwa na Zlatan Ibrahimovic kutokana na ubora wake katika kumiliki mpira, ni sawa na kusema kwamba mashabiki wa Man United wamefurahishwa na usajili wa Joshua Zirkzee.

Zirkzee alikuwa wa kipekee kwa Bologna msimu uliopita, na kwa kuzingatia umri na wasifu wake, 'Mashetani Wekundu' hao wametumia pauni milioni 35 kupata huduma yake inaonekana kama biashara ya bei nafuu.

**5. Leny Yoro kwenda Manchester United (Ada: Pauni Milioni 52.2)**

Pauni milioni 52.2, si ada ya kumlipa kijana wa miaka 18, lakini Leny Yoro anaweza kuwa maalum.

Pamoja na kuwa na uwezo sawa wa kumiliki mpira, Man United wamepata huduma ya mchezaji ambaye anaweza kuongoza safu ya ulinzi ya timu hiyo kwa miaka 15 ijayo.

Unapozingatia hilo, labda si bei mbaya baada ya yote.

**4. Joao Palhinha kwenda Bayern Munich (Ada: Pauni Milioni 47.1)**

Baada ya kukaribia kusajiliwa katika siku ya mwisho ya majira ya joto - alisafiri kwa ndege kwenda Munich kwa uchunguzi wake kabla ya kujua kuwa mpango haukuweza kukamilika - Joao Palhinha sasa, rasmi ni mchezaji wa Bayern Munich.

Nyota huyo wa Ureno, ambaye alicheza mara nyingi zaidi kuliko mchezaji mwingine yeyote wa Ligi Kuu England kwa miaka miwili iliyopita, ndiye kiungo bora katika safu ya kiungo ya Bayern Munich.

**3. Douglas Luiz kwenda Juventus (Ada: Pauni Milioni 42.4)**

Kumuondoa Adrien Rabiot ilikuwa biashara kubwa yenyewe na Juventus, lakini badala yake na kumchukua Douglas Luiz? Kweli, hiyo ni biashara nzuri ya kushangaza.

Mbrazil huyo alikuwa mmoja wa kiungo bora zaidi katika Ligi Kuu England msimu wa 2023/24, na atakuwa mchezaji ambaye Thiago Motta atajenga safu yake mpya ya kiungo ya Juve.

**2. Michael Olise kwenda Bayern Munich (Ada: Pauni Milioni 50.8)**

Kimsingi kila klabu kubwa barani Ulaya ilitaka kumsajili Michael Olise. Na ukizingatia ukweli kwamba ana umri wa miaka 22 tu, na alifunga mabao 16 katika mechi 14 tu alizoanza msimu uliopita akiwa na Crystal Palace.

Kwa Olise, Bayern wamesajili mchezaji ambaye ana uwezo wa kuwa wa kiwango cha kimataifa, na mchezaji ambaye anaweza kuleta alama nyingi.

**1. Kylian Mbappe kwenda Real Madrid**

Bila shaka uhamisho wa Kylian Mbappe kwenda Real Madrid ndio mkubwa zaidi ya orodha hii. Real Madrid walimsajili mwanasoka bora zaidi duniani kwa uhamisho huru.

## Nukuu

"Kumweka Mbappe katika timu haitakuwa tatizo. Ni muhimu kukumbuka alichosema: Atazoea timu. Jambo la msingi ni kwamba kila mchezaji anatakiwa kuchangia kipaji na ubora katika huduma kwa timu. Wakati mwingine anaweza kucheza upande wa kushoto, wakati mwingine anaweza kucheza katikati," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, alipoulizwa na John Obi Mikel kupitia Obi One Podcast, kuhusu nafasi ya Kylian Mbappe katika kikosi chake.**



"Niliweza kuhisi kuanzia sekunde ya kwanza, hii ni klabu ya ajabu. Ni klabu ya ajabu, kubwa sana, kubwa kuliko nilivyofikiria. Kwangu mimi, ni moja ya klabu kubwa, labda klabu kubwa zaidi. Ili kushinda mataji, unaweza kushinda tu na klabu kubwa zaidi, ndiyo maana niko hapa, sisemi tutashinda kila taji, lakini tukifanya kazi kwa bidii tunaweza kufikia na kuwa na chaguzi za kufanikiwa," **Kocha wa zamani wa Bayern Munich na Ujerumani, Hansi Flick, baada ya kuwasili rasmi kuinoa Barca.**



"Ninaweza kusema Vini Jr anastahili kubeba tuzo ya Ballon d'or kwa mwaka huu, kwa sababu amekuwa na mchango mkubwa katika timu yake," **mshambuliaji wa zamani wa Real Madrid, Karim Benzema, akimtabiria nyota wa timu hiyo na Timu ya Taifa ya Brazil, Vinicius Junior, kutwaa Ballon d'or.**





Kipa wa Yanga na Timu ya Taifa ya Mali, Djigui Diarra, akiokoa moja ya michomo ya hatari iliyoelekezwa langoni mwake katika moja ya mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita.

# MAKIPA WA KIGENI WA8 WATAKAOITEKA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KUTAKUWA na ongezeko kubwa la makipa wa kigeni msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Inaonekana baadhi ya klabu za Ligi Kuu nchini zimeamua kusaka magolikipa kutoka nje ya nchi kutokana na sababu mbalimbali.

Hili lilianza kuonekana tangu msimu uliopita, ambapo klabu zote kubwa nchini zilikuwa na makipa wa kigeni, na msimu huu tayari wengine wameshatua nchini.

Sababu zilizotajwa ni kwamba soka hivi sasa limebadilika, ambapo umahiri wa makipa si kuruka tu na kuokoa michomo, bali kuwa na uwezo wa kuchezea miguuni kama mchezaji wa ndani ili kuweza kuanzisha au kuandaa mashambulizi kutoka nyuma.

Makipa wengi wa nje kwa sasa wamekuwa hivyo kutokana na mafunzo wanayoyapata, tofauti na wa hapa ambao wengi hawawezi kuwa na utulivu na mpira miguuni, huku sababu nyingine ikitajwa baadhi yao kutokuwa waadilifu.

Katika makala haya Nipashe linakuletea baadhi ya majina ya makipa wa msimu uliopita na wapya, ambao watasimama langoni msimu ujao kwenye timu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara.

**1. Djigui Diarra - Yanga**

Anatajwa kuwa ndiye kipa bora zaidi

Pia ana uwezo mkubwa na 'taimingi', ambapo ni mara chache sana kuona amezubaa na kubaki langoni kusubiri hatima ya anayeukimbilia, badala yake amekuwa na uwezo wa kutoka na kuweza kuuwahi mpira kabla haujafikiwa na mlengwa.

Raia huyu wa Mali, ni mmoja wa makipa wageni aliyesababisha kuletwa makipa wengi kwenye Ligi Kuu msimu uliopita na utakaonza kutokana na kuwa na vitu vingine ambavyo magolipa wa Kitanzania hawana.

Alijiunga na Yanga mwaka 2021, akitokea klabu ya Stade Malien ya nchini Mali.

**2. Ayoub Lakred - Simba**

Ni mmoja wa makipa waliojipatia sifa kubwa msimu uliomalizika akiwa na Klabu ya Simba. Lakred, raia wa Morocco alisifika kwa uokoaji wake hasa akiwa ana kwa ana na wachezaji wa timu pinzani, akageuka kuwa mhimili mkubwa kwenye timu hiyo.

Ni mmoja wa makipa bora nchini, ambapo pia ana uwezo wa kuanzia mashambulizi kutoka nyuma.

Kutokana na umahiri wake aliouonyesha kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika, haikushangaza kuona Simba ikimwongeza tena mkataba wa mwaka mmoja kuendelea kusalia.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa ameumia akiwa kambini nchini Misri, lakini pia ameongezeka uzito, hivyo itamchukua muda kuwa fiti na kurejea langoni, lakini anatarajiwa kuwapo msimu ujao.

**3. Ley Matampi - Coastal Union**

Matampi ndiye kipa aliyekaa langoni bila kuruhusu bao mara nyingi zaidi kuliko kipa mwingine yeyote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita.

Ni golikipa wa Coastal Union raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambaye amefanya vema msimu mmoja tu tangu atue kwenye kikosi hicho na kukipeleka kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Takwimu zake zinaonyesha kuwa msimu uliopita alicheza mechi 24, sawa na dakika 2160, alipigiwa mashuti 217 langoni mwake, 86 yakilenga lango, aliokoa michomo 75, huku 11 yakitinga wavuni, akiwa na 'clean sheets, 15.

Umahiri wake umesababisha timu nyingi za daraja la Coastal Union nazo kuanza kusaka makipa wageni kuelekea msimu ujao.

**4. Allain Ngeleka - Dodoma Jiji**

Katika kile kinachoonekana makipa wa kigeni wameanza kuwa dili nchini, Dodoma Jiji imeenda kumng'oa kipa Allain Ngeleka raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kutoka Kagera Sugar.

Ni kipa ambaye kwa kiasi kikubwa ameisaidia sana Kagera Sugar kubaki Ligi Kuu kutokana na uwezo wake mkubwa aliouonyesha.

Wala haikushangaza msimu mmoja tu aliosajiliwa na Kagera Sugar kutokea Tabora United na kabla ya hapo alikuwa akikipiga katika klabu ya Lumwana Radiant ya nchini Zambia, huku pia akiwa amewahi kuzichezea Klabu za Nkana Red Devils na Buildcom zote za Zambia, Sanga Balende, Groupe Bazano na Tshinkunku zote na DR Congo, kuchukuliwa na Dodoma Jiji.

**5. Mohamed Kamara - Singida Black Stars**

Hivi karibuni, Klabu ya Singida Black Stars, ilimtangaza kipa raia wa Sierra Leone, Mohamed Kamara, ambaye ametokea Klabu ya Horoya ya Guinea.

Kipa huyo anatarajiwa kuleta ushindani mkali kwa makipa wa Kitanzania watakaokuwa kwenye kikosi hicho, wakiongozwa na Metcha Mnata.

Kamara anayechezea pia Timu ya Taifa ya Sierra Leone, ni mmoja wa makipa wapya wanaotarajiwa kuonyesha vionjo vipya kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

**6. Moussa Camara - Simba**

Imeelezwa kuwa Klabu ya Simba ipo mbioni kukamilisha usajili wa kipa Moussa Camara baada ya kuonekana Ayoub hatopona na kuwa fiti mapema kwa hivi karibuni.

Kipa huyo raia wa Morocco ambaye aliumia akiwa kwenye maandalizi ya msimu mpya, pia ameonekana kuongezeka uzito kitu ambacho kinawatisha viongozi wa Simba na kuona anaweza kuzikosa mechi nyingi za mwanzo wa msimu, hivyo kufanya mazungumzo na kipa huyo anayechezea Timu ya Taifa ya Guinea na alikuwapo kwenye AFCON ya 2023 iliyopita nchini Ivory Coast, lakini akikipiga kwenye Klabu ya Horoya.

Chanzo kinasema huenda jina la Ayoub likatolewa kwenye orodha ya wachezaji wa Ligi Kuu na kubaki kimataifa ambako hakuna kanuni ya idadi ya wachezaji wa kigeni hadi kipindi cha dirisha dogo litakapoamua vinginevyo.

**7. Fabien Mutombora - KMC**

KMC nayo haiko nyuma kuelekea msimu ujao, tayari imeshusha kipa raia ya Burundi, Fabien Mutombora, aliyekuwa akiichezea Klabu ya Vital'O ya Burundi.

Atakuwa mmoja wa makipa wa kigeni ambao wameanza kumiminika kwa kasi nchini kuwapa changamoto makipa wazawa ambao wengi wao wamekuwa hawana mwendelezo katika mechi wanazocheza, baadhi wakicheza vema, lakini zingine wakifungwa mabao mepesi, huku wakifanya makosa mengi.

**8. Mohamed Mustafa - Azam FC**

Baada ya kuhangaika kupata kipa bora kwa muda mrefu, kipindi cha dirisha dogo msimu uliopita, Azam ilimleta golikipa Mohamed Mustafa kutoka El Merrikh ya Sudan.

Ilimuona wakati Yanga ikicheza dhidi ya timu hiyo kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo ikamchukua kwa mkopo.

Kwa nusu msimu tu aliocheza alionyesha uwezo mkubwa na kupigiwa saluti na mashabiki wengi wa soka nchini kiasi cha Azam kuamua kumsajili moja kwa moja kwa misimu miwili.

Anatarajiwa kuwa mmoja wa makipa wa kigeni watakaotikisa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

**JE, WAJUA?**



HUKU akiwa miongoni mwa wanaopewa nafasi ya kutwaa Ballon d'Or 2024, nyota wa Manchester City na Hispania, Rodri, akiwa na timu hizo hadi sasa amecheza michezo 63, amefunga mabao 12, ametoa pasi za mwisho 14. Makombe aliyobeba ni Ligi Kuu England, Uefa Super Cup, Klabu Bingwa Dunia na Euro 2024.

**HABARI KITAIFA**

# Watakiwa kukamilisha ujenzi jengo la wizara

**Na Paul Mbeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhakikisha linakamilisha mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya wizara hiyo lililopo mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma katika muda uliopangwa.

Gugu alitoa agizo hilo juzi baada ya kukamilika kwa kikao kazi baina yake na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Wizara ya Ujenzi pamoja na Wakala wa Majengo (TBA) na baadaye kutembelea mradi huo kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo.

Katika ziara yake aliagiza kuwa ujenzi wa jengo hilo ukamilike ndani ya siku 66 zilizobaki, ili kutimiza lengo na dhamira ya serikali ya kuhakikisha miradi mbalimbali inakamilika kwa wakati.

"Mkataba huu unafikia ukomo kwa vile kukamilishwa unatakiwa kukamilika ifikapo Septemba 30, mwaka huu kwa hiyo kwa siku 66 zilizobaki bado kuna uwezekano wa kutimiza adhma na dhamira ya serikali.

"Pamekuwa na changamoto ya mradi huu kushindwa kukamilika kwa wakati kulingana na muda uliopangwa kimkataba, lakini kwa vile changamoto zilizojitokeza zilikuwa nje ya uwezo wa wizara na mkandarasi ambaye ni NHC tuliweza kuongeza mkataba," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Hamad Abdallah, aliahidi kuukamilisha ujenzi huo kwa viwango ambavyo imekubaliana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuongeza saa za kufanya kazi, ili ukamilike ndani ya siku zilizoagizwa. "Mimi kama kiongozi nitahakikisha timu yangu inafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha dhamira ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya kupata jengo zuri lenye viwango linatimia," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Wizara ya Ujenzi Utawala na Rasilimaliwatu, Mrisho Mrisho ambaye alimwakilisha katibu mkuu wa wizara hiyo, alisema wizara itaendelea kusimamia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ili ahadi iliyotolewa kwa katibu mkuu kutekelezwa kwa wakati

Msanifu Majengo, Victor Baltazar kutoka wakala wa majengo Tanzania (TBA) alisema Wakala wa Majengo Tanzania itatoa ushirikiano wa karibu na kutatua changamoto zote zilizosababisha mradi kusuasua na kuhakikisha kazi hiyo inakamilika ndani ya muda uliopangwa.



Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Udhibiti wa Taka Ngumu jijini Dodoma, Dickson Kimaro, akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Mwaja, Kata ya Chamwino jijini humo, kufanya usafi ili kuepukana na magonjwa, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Teknolojia ya masafa ardhini kutumika kutafuta maji Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema serikali itashirikiana na Kampuni ya Al Fradaws Investment Company Limited ya nchini Jordan kutumia teknolojia mpya ya masafa ya ardhi (Radio Frequency Technology) kwa ajili ya kutafuta maji chini ya ardhi, ili kuondoa tatizo la ukosefu wa maji katika baadhi ya maeneo nchini.

Aliyasema hayo jana baada ya kutembelea mashamba ya uzalishaji mbegu katika Kijiji cha Choda wilayani Ikungi ambako kampuni hiyo imewekeza katika kilimo cha umwagiliaji, kwa kuja na teknolojia mpya ya kutafuta maji chini ya ardhi itakayoleta suluhisho la upatikanaji wa maji kwa njia rahisi. Aweso alisema baadhi ya maeneo nchini kama vile Tunduma mkoani Songwe, Kiomboi wilayani Iramba na Ngerengere yana changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji kwa sababu teknolojia inayotumika na kutambua eneo maji yapo kabla ya kuchimba kisima haileti msaada sana katika baadhi ya maeneo hayo.

Alisema teknolojia mpya ya radio frequency iliyoletwa na Kampuni ya Al Fradaws Investment ambayo inaonyesha wapi maji yalipo, umbali gani yanapatikana, uwingi wa maji na ubora wa magics, itakwenda kuondoa tatizo la ukosefu wa maji kwenye maeneo yenye changamoto nchini.

"Hakuna sababu yeyote ya Watanzania kufa sababu ya ukosefu wa maji, kupitia teknolojia hii tunakwenda kumaliza tatizo la maji maana teknolojia tuliyonayo ambayo tunaitumia kama wizara kunakuwa na changamoto ya kupata maji katika baadhi ya maeneo," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Al Fradaws Investment, Ahmed Alkhatib, alisema teknolojia wanayoitumia kupata maji ni ya kisasa na ya uhakika hakuna kukisia vyombo wanavyotumia vikionesha eneo fulani kuna maji inakuwa ni uhakika asilimia 100.

Alisema katika nchi nyingi ambazo wamepeleka teknolojia hii mpya wamebaini serikali zinaingia mikataba na makampuni kwa kutafuta maji kwa teknolojia ya jiolojia yaani 'topography', ambayo wakati mwingine inakuwa na changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo yanayochimbwa visima vya maji.

"Sisi teknolojia tunayoitumia ni ya masafa ardhini hivyo tuna uwezo wa kuona maji chini ya ardhi hatukisii, tukajua uwingi wa maji, umbali yanapopatikana na ubora kama yana chumvi au hayana," alisema.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema kampuni hiyo imewekeza mashamba kwa kupewa hekta 10,000 katika Kijiji cha Choga ambapo michakato ya kutoa eneo hilo la ardhi ilifanyika kwa kushirikisha serikali ya kijiji.

Alisema katika teknolojia mpya ya kutafuta maji iliyoletwa na kampuni hiyo wana mitambo ambayo inaweza kuchimba maji chini ya ardhi hadi kilometa moja na wametengeneza gari ambalo lina uwezo wa kuchimba maji kwenda chini zaidi ya mita 700.

Kijazi alisema teknolojia hiyo ni muhimu sana inatawezeza kuleta suluhisho la ukosefu wa maji katika baadhi ya maeneo na hasa ikizingatia kuwa Tanzania hatuna uwezo wa kuchimba maji chini ya ardhi za mita 300.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

**Jina la awali la kituo:** Mkombozi Na Ngemelo Petrol Station
**Nambari ya Leseni:** PRLR-2022-016
**Mahali Kituo kilipo:** Kijiji cha Nyamwage, Kata ya Mbwara, Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani
**Jina linalopendekezwa:** Mabena Filling Station
**Mmiliki wa awali:** Mkombozi Kusana Mbutila
**Mmiliki mpya:** Amos Site Mabena

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA
Jengo la EWURA, 3 Barabara ya EWURA, 41104 Tambukareli,
S. L. P. 2857
DODOMA

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz





# TARURA yatia saini mkataba utekelezaji miradi mitatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), umetia saini mikataba mitatu ya ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mkoa wa Mbeya, Soko la Kisasa na barabara za mitaa kwa kiwango cha lami ambayo inadaiwa itabadili taswira ya jiji hilo na kuongeza mapato.

Mikataba hiyo ilisainiwa juzi baina ya TARURA na makandarasi mbalimbali na kushuhudiwa na viongozi mbalimbali wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.

Kwa mujibu wa taarifa ni kwamba inatekelezwa kupitia mradi wa kuboresha miundombinu katika miji, manispaa na majiji (TACTICS) na kwamba ujenzi wa kituo cha mabasi pamoja na soko la Sokomatola vitagharimu Sh. bilioni 30 huku barabara za mitaa zenye urefu wa kilomita 23 utagharimu Sh. bilioni 21.58.

Waziri Mchengerwa alimtaka Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya kwa kushirikiana na watendaji wa TARURA wa jiji hilo kusimamia vizuri miradi hiyo, ili ikamilike kwa wakati na kwa viwango vilivyoko kwenye mikataba kulingana na fedha iliyotengwa. Vilevile alimtaka mkandarasi anayetekeleza miradi hiyo kuhakikisha anakamilisha ndani ya muda ulioko kwenye mkataba ambao ni miezi 15 ili ianze kutumika.

"Lakini naagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini ambako miradi hii inatekelezwa kuhakikisha wanasimamia vizuri, ili kuhakikisha inajiendesha yenyewe na kuongeza mapato hasa masoko na vituo vya mabasi," aliagiza Mchengerwa.

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seff alisema mradi wa TACTICS unatekelezwa katika miji 45 yakiwamo majiji matano na kwamba fedha za utekelezaji zinatokana na mkopo wa Sh. trilioni 1.16 kutoka Benki ya Dunia (WB).

Alisema kwa Jiji la Mbeya, mradi huo mbali na ujenzi wa kituo cha mabasi na soko la Sokomatola pia kuna barabara tisa za mitaa zitajengwa pamoja na mifereji ya maji ya mvua.

Seff alisema soko pamoja na kituo cha mabasi vitajengwa na Kampuni ya Sihotech Engineering Company LTD and AMJ Global Mult Contractors Company LTD.

"Lakini kwenye mradi huu pia kuna kipengele cha kuzijengea uwezo taasisi zote kwa maana ya wizara, Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) na halmashauri kuhusu kuboresha utendaji kazi, ufanisi wa huduma kwa jamii pamoja na ununuzi wa vitendea kazi yakiwamo magari ya usimamizi," alisema Seff.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, aliishukuru serikali kwa kuanza utekelezaji wa miradi hiyo akidai kuwa itasaidia kuboresha mweonekano wa jiji hilo pamoja na kuboresha huduma za jamii.

Alisema pamoja na mradi huo pia serikali imeboresha miundombinu mbalimbali ndani ya jiji hilo ikiwamo ujenzi wa Daraja la Mwasanga ambalo kwa sasa limekamilika na wananchi wanalitumia. Alisema kabla daraja hilo halijajengwa, wananchi walikuwa wanatumia daraja la kienyeji ambalo lilibomoka na kusababisha vifo vya watu watano ambao walikuwa wanavuka.

Aidha, aliiomba serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara jijini humo kwa maelezo kuwa lina barabara za mitaa zenye urefu wa zaidi ya kilomita 400 ambazo zinatakiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kwa mwaka wa fedha uliopita Jiji la Mbeya lilipokea zaidi ya Sh. bilioni 30 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa (katikati), akikata utepe kuzindua mikataba ya ujenzi wa barabara za mitaa, kituo kikuu cha mabasi cha Mkoa wa Mbeya na Soko la Sokomatola kabla ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo, TARURA na makandarasi jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC Mtaka aeleza namna barabara za zege zinavyotumia fedha nyingi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amesema ujenzi wa barabara ya Itoni - Lusitu kwa kiwango cha zege yenye urefu wa kilometa 50 inagharimu fedha nyingi ikilinganishwa na barabara ya lami lakini faida yake ni kubwa zaidi.

Barabara hiyo inatajwa kuwa itagharibu Sh. bilioni 120 na kwamba ni sehemu ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (Km 211.4).

Mtaka aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua mradi wa barabara kipande cha Itoni-Lusitu unaotekelezwa na mkandarasi M/s China Civil Engineering Construction Cooperation.

"Gharama ya kujenga kilometa moja ya barabara ya zege Ludewa, unaweza kujenga wastani wa kilometa tatu mpaka nane kwenye barabara za kawaida za lami kwa sababu kilometa moja ya barabara ya zege ni Sh. bilioni 1.8 wakati sisi kwenye barabara ya lami hizi za kawaida tunajenga kwa wastani Sh. milioni 600 hadi 800," alisema Mtaka.

Aidha, alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha barabara yote ya Ludewa inajengwa kwa kiwango cha zege na kukamilika kwa wakati, ili kutoa huduma kwa wananchi pamoja na wawekezaji.

"Kwa hiyo miradi hii inapojengwa watu wote wanaotokea Njombe, watu wote wanaotokea Ludewa waanze kuangalia ni fursa zipi za uwekezaji zitakazojitokeza baada ya barabara hizi kukamilika," alisema Mtaka.

Alisema wananchi mkoani Njombe wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kukwamua mradi wa Liganga na Mchuchuma ambao kwa miaka zaidi ya 40 umezungumzwa kwenye maneno na haukuonyesha utekelezaji wake.

"Ametekeleza kwa vitendo kwanza kwa kulipa fidia, pili kwa kujenga miundombinu ya barabara ya zege ambayo imekuwa kikwazo kwa wakati wote kupata wawekezaji kwenye maeneo hayo," alisema Mtaka.

Meneja wa Wakala wa Barabara TANROADS Mkoa wa Njombe, Mhandisi Ruth Shalua alisema mradi wa barabara Itoni-Lusitu umefikia asilimia 23 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka huu.

"Uimara wa barabara hii ni TLC 50 inamaana kwamba tunauhakika barabara yetu inaweza ikapitisha magari yenye uzito mpaka tani 50, lakini tunategemea ukomo wa barabara uwe ni miaka 50," alisema.

Alisema serikali imejenga barabara hiyo kwa kiwango cha zege kwa sababu inampango mkubwa wa kuwekeza katika makaa ya mawe na chuma.

# Wenye ulemavu walia sheria kutozingatiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wenye ulemavu mkoani Mbeya, wamesema licha ya Bunge kutunga sheria maalumu ya kutambua haki zao ya mwaka 2010, bado baadhi ya viongozi wa serikali wamekuwa wagumu kutekeleza sheria hiyo na hivyo kuwanyima haki.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu Tanzania (CHAWATA) Mkoa wa Mbeya, Damas Mwambenje, aliyasema hayo juzi wakati wa Kongamano la Katiba lililoitishwa na Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA) na kushirikisha makundi maalumu ya jamii.

Makundi yaliyoshiriki kwenye kongamano hilo ni watu wenye ulemavu, mama lishe, waendesha pikipiki (bodaboda) na waendesha pikipiki za magurudumu matatu maarufu bajaji.

Mwambenje alisema baadhi ya viongozi wa serikali wamekuwa wakizitoa haki hizo kama hisani na kwamba endapo mtu mwenye ulemavu hapatani na kiongozi husika basi huwa hawezi kupata haki hizo jambo ambalo ni kinyume na sheria hiyo.

Alizitaja baadhi ya haki ambazo wamekuwa wakizikosa ni pamoja na kupatiwa vifaa vya utengamao kwa watu wenye ulemavu hasa watoto pamoja na huduma yenyewe ya utengamao.

Aidha, alisema vifaa hivyo vinauzwa gharama kubwa na baadhi ya watu wenye ulemavu wanaoishi maeneo ya vijijini wamekuwa wakivikosa kutokana na umbali wa maeneo yenyewe na gharama kuwa kubwa.

"Tunaomba hizi haki zetu ziainishwe kabisa kwenye katiba ili na sisi tuwe na nafasi ya kuchukua hatua pale tunapoona hatutendewi haki ipasavyo, kuna baadhi ya watoto maeneo ya vijijini wanazidi kuwa walemavu kwa sababu ya kukosa vifaa vya utengamao," alisema Mwambenje.

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania Mkoa wa Mbeya, Tusajigwe Mwalweja alisema katiba inayotumika ya Mwaka 1977 inawanyima haki ya kuajiriwa kwenye taasisi za umma kama ilivyo kwa watu wengine.

Alisema baadhi ya watu wenye ulemavu wakiwamo wa viungo na wenye ualbino wamekuwa wakipata ajira kirahisi tofauti na ilivyo kwa viziwi akidai kuwa wamekuwa wakitengwa.

Hata hivyo, alisema hata kwenye nafasi za kisiasa zikiwamo za ubunge na udiwani, viziwi wamekuwa wakiwekwa kando huku watu wenye ulemavu wa aina nyingine wakichaguliwa ama kuteuliwa.

"Kwa hiyo na sisi tunataka katiba ambayo itatuhusu, tunashukuru Jukwaa la Katiba wametusaidia kuja kutufungua macho kwa sababu kuna mambo mengi tulikuwa hatuyajui lakini kupitia hili tumeanza kujua," alisema Tusajigwe.

Meneja wa Mradi wa Elimu Jumuishi ya Child Support Tanzania (CST), Nemes Temba ambaye ni mwenye ualbino alisema watu wenye ulemavu wamekuwa wakionekana kwenye jamii kama sio watu wa kawaida.

Alisema hali hiyo ndiyo ambayo huwa inasababisha unyanyapaa kwenye jamii na hivyo akaiomba serikali kuweka mizingi imara kwenye katiba itakayowalinda watu wa kundi hilo.



# RC aeleza namna mkonge utakavyobadili maisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema matumizi ya bidhaa za mkonge zitabadilisha maisha ya wajasiriamali wa Zanzibar.

Akizungumza jana katika eneo la Makunduchi mkoani humo wakati wa uzinduzi wa ubunifu, usarifu na matumizi ya bidhaa za mkonge, alisema matumizi ya bidhaa za mkonge yamekuja baada ya kuonekana kuna upungufu wa matumizi ya bidhaa zitokanazo na mnazi ikiwamo makumbi kwa ajili ya kutengeneza kamba ya usumba.

Alisema kutokana na upungufu huo sasa wanawashajihisha wajasiriamali wanaotumia kamba za usumba kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali, ikiwamo mikoba kutumia kamba za mkonge ili kuendeleza biashara zao za kujipatia kipato.

Alisema kuwa kabla ya kuja na matumizi ya kamba za mkonge kumefanyika utafiti na kubainika kuwa kamba hizo ziko salama kwa matumizi hayo na imeonesha kuwa inafaida kubwa tofauti na kamba ya usumba.

Aidha, alisema matumizi ya kamba za mkonge yapo imara katika kuandaa vifaa mbalimbali ikiwamo mikoba, hivyo ni vyema wananchi kutumia vyema bidhaa hiyo ili izidi kuwaletea maendeleo.

Mkuu huyo alisema katika matumizi hayo lazima wajasiriamali wawe wabunifu kwa kile wanachokifanya, ili kuendana na wakati uliopo na utafutaji wa masoko ya ndani na nje.

Aidha, alisema katika kufikia maendeleo juu ya matumizi hayo ya mkonge serikali ya mkoa imepanga kutoa elimu kwa wajasiriamali wote watakao tumia kamba hizo na kuwatafutia masoko ya uhakika ili kukuza vipato vyao.

Alisema Bodi ya Mkonge Tanzania imeona kunahaja kubwa ya kuleta bidhaa hiyo visiwani humo kwa sababu ya kuunga mkono jitihada za serikali za kuwapatia maendeleo wananchi wake. Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania, Sadi Kambona, alisema bodi hiyo imekabidhi tani tisa za nyuzi za mkonge kwa Chuo cha Mafunzo (Magereza) zenye thamani ya Sh.milioni 40 kwa lengo la kukabidhi vikundi 20 vya wajasiriamali wa Mkoa wa Kusini Unguja kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na bidhaa hiyo.

Aidha, alisema mazao ya mkonge yanafaida kubwa katika kukuza uchumi wa mtu na taifa kutokana na uzalishaji wake kuonekana unasoko kubwa ndani na nje ya nchi.

Alisema mwaka 2020 soko la ndani lilikuwa ni shilingi bilioni saba na soko la nje lilifikia dola milioni 5.78, huku mwaka 2023 soko la ndani lilikuwa Sh. bilioni 3.3 na soko la nje lilikuwa dola milioni 2.74.

Alisema maamuzi ya kuleta bidhaa hiyo Mkoa wa Kusini Unguja ni kuwafanya wajasiriamali kutumia bidhaa hiyo kwa ufanisi kutokana na bidhaa zake zinasoko kubwa Ulaya, hatua ambayo itawawezesha wananchi wa visiwa hivyo kupiga hatua kubwa ya maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

Akizungumza chimbuko na uhusiano wa uzinduzi huo Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar (magereza), Khamis Bakar alisema chimbuko la matumizi ya bidhaa hiyo ni kutokana na chuo hicho kuanzisha kituo cha mafunzo ya ujasiriamali na kuja na wazo la ubunifu na matumizi ya bidhaa zitokanazo na mkonge.

Alisema hali hiyo ilìwapelekea wafungwa kwenda Tanga kujifunza juu ya uzalishaji wa bidhaa hiyo, na kwamba baada ya kufanya tafiti walibaini kwamba bidhaa hiyo inauhitaji mkubwa nchini kutokana na kupungua kwa bidhaa zitokanazo na kamba za usumba.

Mkurugenzi Idara ya Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Abdulla Mohamed Juma, alisema suala la mkonge linakwenda sambamba na shughuli za utalii kwasababu watalii wengi hupenda vitu vinavozalishwa na mnazi, lakini mnazi hivi sasa imekuwa ni changamoto hivyo kuja kwa bidhaa hiyo nchini itaongeza fursa ya bidhaa za kitalii zitokanazo na bidhaa hiyo.

Wakizungumza baadhi ya wajasiriamali katika koa huo, walisema matumizi ya kamba ya mkonge yameonekana ya haraka zaidi na vitu vyake kuwa na ubora tofauti na kamba ya usumba.

# ACT-Wazalendo Zanzibar wataka mabadiliko sheria kura ya mapema

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema Zanzibar hakutakuwa na uchaguzi wa mwaka 2025, kama sheria ya kupiga kura ya mapema ambayo hupigwa siku moja kabla ya uchaguzi mkuu haitabadilishwa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, wakati akihutubia kwenye mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika kwenye uwanja wa Jadida Jimbo la Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

"Hapa hatutofanya uchaguzi wa siku mbili, na uchaguzi utakaofanyika ni wa siku moja tu, kama wanataka uchaguzi twende kwenye uchaguzi wa huru na wa haki," alisema Othman Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mwenyekiti huyo alisema tangu kuazishwa kwa mfumo wa vyama vingi wananchi wakipata misukosuko na wengine kupoteza maisha na kupata ulemavu kwa sababu ya kutoheshimiwa misingi ya demokrasia na utawala bora wakati wa uchaguzi.

Akizungumzia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, alisema Zanzibar itaendelea kubaki maskini kwa sababu mambo ya kimsingi ya kiuchumi karibu 41 yameingizwa katika orodha ya mambo ya muungano.

Aliyataja baadhi ya mambo hayo ni bandari, ushuru wa forodha, usafiri wa anga, elimu ya juu, fedha na sarafu, mambo ya nje, uhamiaji, mafuta na gesi pamoja na mmalaka ya hali ya hewa na uvuvi wa bahari kuu. Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, alisema viongozi na wanachama wa chama hicho wamejifunza siasa kutoka kwa aliyekuwa mwanasiasa mkongwe marehemu Maalim Seif Sharif Hamad.

Alisema kwamba inasikitisha makubaliano yaliofikiwa kabla ya kuundwa kwa serikali ya umoja wa kitaifa mwaka 2020 mpaka sasa hayajatekelezwa wakati Zanzibar inaelekea katika uchaguzi mkuu mwakani.

Hata hivyo, alisema nguvu za Chama cha ACT-Wazalendo zitaonekana katika kisanduku cha kura mwakani na tayari wamejipanga kuhakikisha kila mwananchi anapata haki ya kuandikishwa na kupiga kura kwa sababu ni haki yake ya kikatiba na kisheria.

Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Masour Yussuf Himid, alisema ni muhimu hoja zao zikajibiwa kwa hoja kwa ajili ya manufaa ya wananchi wote.

Aidha, aliwataka wafuasi na wanachama wa ACT-Wazalendo kujenga umoja na mshikamano bila ya kutetereka, ili kufikia malengo ya kushika madaraka yalioazishwa na Marehemu Seif Sharif Hamad.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na wajumbe wa sekretarieti ngazi za matawi, wadi na majimbo katika mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo wajumbe hao, yaliyofanyika katika ukumbi wa Umoja ni Nguvu, Mkoa wa Kusini Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahamasisha wanawake kushiriki siasa kwa maendeleo ya utawala bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, amesema ushiriki wa wanawake katika siasa ni muhimu kwa ajili ya usawa wa kijinsia na utawala shirikishi.

Aliyasema hayo Visiwani Zanzibar juzi, wakati akifungua kikao cha mazungumzo kuhusu ukatili dhidi ya wanawake kwenye uwanja wa siasa, kikao ambacho kimeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Babari Wanawake Tanzania (TAMWA Zanzibar) kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Demokrasia (NDI) chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani USAID.

Alisema wanawake katika majukumu ya kisiasa huleta mitazamo ya kipekee na uzoefu ambao husababisha sera za kina zaidi ambapo utofauti huo katika uwakilishi unahakikisha kwamba mahitaji na haki za raia wote zinashughulikiwa.

Naibu waziri huyo alisema ushiriki wa wanawake katika siasa huhamasisha vizazi vijavyo kutamani nafasi za uongozi, na kukuza utamaduni wa usawa wa kijinsia.

"Zaidi ya hayo ushiriki wa wanawake katika siasa huimarisha demokrasia kwa kukuza uwazi na uwajibikaji. Viongozi wanawake mara nyingi hutanguliza masuala ya kijamii kama vile elimu, afya, na ustawi wa familia, ambao hunufaisha jamii kwa ujumla," alisema.

Aidha, alisema ushiriki wao katika michakato ya kufanya maamuzi huhakikisha kwamba sauti za wanawake na makundi yaliyotengwa zinasikika, na hivyo kusababisha matokeo ya usawa zaidi.

Hata hivyo, alivitaka vyama vya kisiasa na asasi za kiraia zichukue msimamo dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na vyama vya kisiasa vinapaswa kupitisha na kutekeleza kanuni za maadili zinazokataza vurugu na unyanyasaji.

"Ni lazima watoe mafunzo kwa wanachama kuhusu usikivu wa kijinsia na utatuzi wa migogoro. Zaidi ya hayo, wahusika wanapaswa kuunda mifumo ya ndani ya kuripoti na kushughulikia matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake," alisema.

Aidha, alisema ushirikiano kati ya vyama vya siasa na AZAKI ni muhimu kwa ajili ya kujenga mazingira salama na ya kusaidia wanawake katika siasa.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema wamefanya tathmini ya wanawake kushiriki katika vyama vya siasa kwa kuchagua na kuchaguliwa, ili kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi.

Alisema ingawa wanawake wagombea majimboni na baadhi yao kushinda, lakini bado kuna changamoto ikiwamo hofu kwa wanawake, udhalilishaji wa kijinsia na kupelekea ushiriki wao ni mdogo katika vyombo vya maamuzi.

Aidha, aliitaka ofisi ya mrajisi wa vyama vya siasa kuhakikisha kuna ripoti nzuri ya masuala ya maendeleo ya kijinsia kutoka katika vyama vya siasa, ikiwamo vyama kuwa na bajeti inayohusiana na masuala ya wanawake ili kuwa na usawa wa kijinsia.


Abrazak Said Ali Mwanasheria kutoka ofisi ya msajili wa vyama vya siasa, alisema marekebisho makubwa yamefanyika katika sheria ya vyama vya siasa hasa katika kifungu cha 10 (C) ambapo imeilazimu kila chama cha siasa kuwa na sera za jinsia ambapo vyama vingi vilikuwa havina sera hiyo.

Alisema imefika wakati nafasi za viti maalum kuwa ni nafasi za kujifunza na badala ya hapo wanawake kwenda majimboni kugombea nafasi za uongozi badala ya kuishia katika nafasi hizo za viti maalum.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA CHETI



**THECLA WILLIAM MGEMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha eliimu ya darasa la saba cha mtoto wake aitwae **JEFFERSON JALPHARY DONGE** namba ya mtihani **PS2402028/00020**, namba ya cheti 0794934. Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EMAU ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL** mwaka 2017, Cheti hiki kimepotea mkoani MWANZA. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MWA/ILE/26649/2024.**

### KUPOTEA KWA VYETI



**TIBERA KAGEMULO RUGAMBWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0239-0075** kiilchotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. FRANCIS GIRLS SECONDARY SCHOOL** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0800-0585** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **LOYOLA HIGH SCHOOL** na cheti cha chuo chenye usajili namba 2008-02-00713 kilichotolewa na **MUHIMBILI UNIVERSITY OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES (MUHAS).**
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/154433/2024**
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/154436/2024**

### KUPOTEA KWA VYETI

**MKUU WA SHULE NGYEKU SEKONDARI ,** AMEPOTELEWA NA BAHASHA ILIKUWA IMEBEBA VYETI **40 (AROBAINI)** VYA WATAHINIWA KIDATO CHA NNE, **MWAKA 2020.** KWA YEYOTE ATAKAYEONA HIYO BAHASHA TUNAOMBA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0769743466/0658743466 .**
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/MER/24489/2024**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMIS SADIKI SHEKIMWERI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI** 6D14 yenye usajili namba **T 143 AFB,** CHASSIS NAMBA **FM515J50031** na ENGINE NAMBA: **6D14414899.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/155285/2024**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CYPRIAN JONATHANI MANGUGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 617 CFE,** CHASSIS NAMBA: **SXA110071692** na ENGINE NAMBA: **3S6928304.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/152006/2024**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RUSIAN ISTORY KILUMILE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI CANTER yenye namba **T 498 DFH,** CHASSIS NAMBA: **FE638EV420374** na ENGINE NAMBA: **3JTFE374.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/RUV/MAD/4364/2024**

### TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki wa Kampuni ya **SHUKURU INC. LIMITED** iliyosajiliwa kwa namba **152366825** Tarehe 21/06/2021,Wanapenda kutangazia umma kuwa Wameamua kufunga kampuni hiyo kwa Hiyari,Kwa mujibu wa kifungu cha sheria ya makampuni no.333(1)(b) Sura ya 212 na Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA.)

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No. 16633 of 2024**

**In the matter of the estate of the late SEBASTIAN BONIFACE PETER Of Nzuguni Dodoma**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by REBECA MASAMBAI JUMANNE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of 8....2024

Dated at Dodoma this 25 day of 7....2024

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF TEMEKE DISTRICT AT TEMEKE ONE – STOP JUDICIAL CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6244 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ZEBEDAYO ZAKAYO SEKIRASA**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR PROBATE AND LETTER OF ADMINISTRATION**

**ISRAEL ZAKAYO SEKIRASA.........................PETITIONER**

**NOTICE TO THE CREDITORS**
**(made under Rule 111 of the probate Rules)**

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named **ZEBADAYO ZAKAYO SEKIRASA** deceased, who died at Eudad Hospital Tanzania Kinondoni Dar es salaam on the 14th day of March, 2023 and probate of who's the letters of administration of the estate was granted to me **ISRAEL ZAKAYO SEKIRASA** by the court on the 10th day of june, 2024 are hereby required to send their claims to me **ISRAEL ZAKAYO SEKIRASA** at the following address within thirty (30) days from the date of publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to handover the assets to the person entitled thereto having regard only to the claims of which I shall then have had notice.

ISRAELZAKAYO SEKIRASA
ADMINISTRATOR
Postal office Box No. 33372,
Mobile: 0757 299 606
Dar Es Salaam

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Shauri la mirathi Na 1112/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED SHIJA KAHAMO WA DAR ES SALAAM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA MWANAID HAMIS NASIB**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi katika mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 mwezi 08 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 07 mwaka 2024

HAKIMU

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 17870 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late ANTHONY LUCAS KUNG'ALO**

1. **BY MICHAEL GIMBI KITANZIMA**
2. **AGRIPINA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 15 day of 8 2024

Dated at MOROGORO this 26 day of 7 2024

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660,Morogoro

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA INAYOKETI TABORA**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 328 YA 2019**

**ESTHER KAYAYA.................................MLETA RUFAA**

**DHIDI YA**

**UBANI MANYAMBO...............................MJIBU RUFAA**

**KWA: UBANI MANYAMBO**
**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na mahakama hii hapa Tabora tarehe 5/08/2024 saa tatu kamili asubuhi (3:00) Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi haya hayatasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 22/07/2024

O. H. KINGWELE
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

## HABARI KIMATAIFA

# Vita Israel, Gaza vyaendelea, 170 wauawa, 100 kujeruhiwa

**GAZA,** PALESTINA

WIZARA ya Afya ya Hamas katika Ukanda wa Gaza yabainisha kuwa shambulizi la Israel katikati mwa Palestina limesababisha vifo vya watu 30 na kufikisha idadi ya vifo 170 tangu Julai 22, mwaka huu, 100 kujeruhiwa.

Wizara hiyo ilisema jana kuwa shambulizi hilo lilifanyika katika Shule ya Khadija, ambayo ilikuwa na kitengo cha matibabu cha muda katika eneo la Deir al-Balah, pia limesababisha zaidi ya raia 100 kujeruhiwa.

Kutokana na tuhuma hizo, Jeshi la Israel, lilisema limefanya operesheni katika shule hiyo ikiwalenga magaidi waliokuwa wakiendesha shughuli zao katika eneo hilo.

Wakati huo huo jeshi la ulinzi wa raia la Gaza lilisema operesheni ya Israel inayoendelea tangu Julai 22 huko Khan Younes imesababisha madhara makubwa ndani na nje ya mji huo wenye wakazi wengi kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Katika hatua nyingine, ilielezwa kuwa takriban watu 11 waliuawa baada ya kurushwa kwa roketi kwenye milima ya Golan inayokaliwa na Israel, huku Hezbollah kutoka Lebanon ikihusika na shambulio hilo.

Kwa mujibu wa jeshi la Israel, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alisema vuguvugu la Kiislamu la Lebanon litalipa gharama kubwa kwa shambulio hilo lililoukumba mji wa Kiarabu wa Majdal Shams.

Aidha, Hezbollah, imepinga vikali madai hayo ikikanusha kuhusika na shambulio hilo.

Jeshi la Israel lilisema watu hao 11, wenye umri wa miaka 10 hadi 20, waliuawa wakati roketi ilipopiga uwanja wa mpira wa miguu huko Majdal Shams, huku 19 wakijeruhiwa, kulingana na waokoaji.

"Tutajiandaa kujibu Hezbollah, tunakamilisha tathmini zetu na tutachukua hatua," msemaji wa jeshi la Israel Rear Hagari alisema.

***RFI***




Kamala Harris, makamu wa rais wa Marekani anayekaribia kuteuliwa rasmi kuwa mgombea urais wa Chama cha Democratic. **PICHA: MTANDAO**

# Hamasa ya Kamala yafika Ulaya

**NEW YORK,** MAREKANI

WANAHARAKATI wa Chama cha Democratic barani Ulaya wamesema wapigakura na hata raia ambao si Wamarekani wamepata hamasa mpya kuhusu makamu wa rais wa Marekani, Kamala Harris kugombea urais Novemba 5, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa siku chache zilizopita na msemaji wa Muungano wa Chama cha Democratic nje ya Marekani, 'Democratic Abroad' (DA), Amy Porter.

Tangu uamuzi wa Rais Joe Biden kukabidhi kijiti cha uongozi kwa makamu wake Kamala, Porter alisema muungano huo, unaokiwakilisha Chama cha Democratic ulimwenguni kote, umeshuhudia ongezeko la usajili wa wapigakura wapya na watu wa kujitolea wanaotaka kusaidia kampeni ya mteule huyo.

Alisema hali hiyo ni ya kustaajabisha na ni jambo ambalo pengine ni la kusisimua zaidi, na kwamba wamekuwa na Wafaransa wakiwasiliana nao wakisema wangependa kusaidia kuhakikisha Kamala anachaguliwa.

Katika miongo kadhaa ya kufanya kazi ya kujitolea na muungano huo, Porter alisema amewahi kushuhudia hali hii kwa nadra sana.

Mpango wa serikali ya shirikisho la Marekani wa kusaidia masuala ya upigaji kura unakadiria kwamba kuna Wamarekani milioni 2.8 wanaoishi nje ya nchi ambao wana haki ya kupiga kura katika chaguzi za shirikisho.

Ilielezwa kuwa mwaka 2016, kwa mujibu wa mahesabu ya mpango huo, ni asilimia 6.9 tu kati yao waliopiga kura.

Wafuasi wa Chama cha Democratic wanatumai kwamba sasa fursa hiyo imechochewa na wengi na huenda wakashiriki uchaguzi wa Novemba 5.

Muungano wa DA ulisema usajili wa wapigakura nje ya Marekani kupitia njia ya barua umeongezeka mara tano katika kipindi cha siku tatu wiki hii, hadi kufikia 3,000 ikilinganishwa na kipindi kama hicho wiki iliyopita.

Mchakato huu huwasajili wapigakura wa vyama vyote, lakini muungano wa DA ulisema idadi ya wanachama wake wapya pia iliongezeka mara tatu kutoka Jumatatu hadi Jumatano wiki iliyopita.

"Fedha nyingi zimekuwa zikimiminika katika makasha ya muungano, huwa tunapata michango mara kwa mara, lakini huu umevuka viwango vilivyozoeleka," alisema.

Dana Freling aliasisi tawi la muungano wa Democratic Abroad, DA, nchini Finland baada ya Donald Trump kuingia madarakani mwaka 2017.

Alisema ameshuhudia wimbi la wafanyakazi wapya wa kujitolea katika siku za hivi karibuni, wakiwamo raia wa Finland ambao anasema wana wasiwasi kuhusu hulka ya rais wao wa zamani kuelekea Jumuiya ya Kujihami ya (NATO).

"Usalama wa Finland unategemea jinsi rais wa Marekani atakavyouongoza muungano huu na tunahisi kwamba usalama wetu unategemea na jinsi rais anavyouunga mkono mtandao wa NATO," alisema.

Ingawa sera ya nje haichukuliwi kuwa eneo mojawapo ambalo Kamala ana nguvu, lakini katika mkutano wa kimataifa wa usalama mjini Munich, aliweka bayana maoni yake kuhusu Russia, akithibitisha kuiunga mkono Ukraine na kuwahakikishia washirika kwamba ahadi za utawala wa Biden kwa NATO zinabaki imara.

Freling alisema ongezeko la ghafla la uungwaji mkono kwa urais wa Kamala limefuta uasi wa wapigakura na hata kuwashawishi wafuasi wa Chama cha Republican kama kaka yake anayeishi jimboni Texas wabadili tiketi zao.

Alisema kaka yake alibadilika kutoka mtu aliyempuuzia Kamala hadi kuamua kumpigia kura.

***DW***

# Watu 22 wafariki dunia shambulizi Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

KUNDI moja la wanaharakati wa demokrasia nchini Sudan limesema takriban watu 22 wameuawa baada ya kundi la kijeshi lenye silaha la Msaada wa Haraka (RSF), kushambulia mji wa al-Fashir.

Kundi hilo la 'The al- Fashir Resistance Committee' kupitia ukurasa wake wa Facebook lilisema kuwa wanamgambo wa RSF walirusha makombora kwenye soko, hospitali na makazi ya watu na kwamba pia walitumia droni kulenga hospitali.

Ilielezwa kuwa mji huo ndio wa mwisho unaodhibitiwa na jeshi la serikali kwenye eneo la Darfur, ambalo ni ngome muhimu kwenye vita vyake dhidi ya RSF, ambavyo vimesababisha janga kubwa zaidi la kibinadamu.

Pia kundi hilo lilisema limehesabu miili 22, na kwamba idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka.

Kufikia jana hakukuwa na tamko lolote kutoka RSF, ambalo awali lilikuwa likikanusha madai kama hayo ya kushambulia maeneo ya raia.

Aidha, ilielezwa kuwa zaidi ya watu 300,000 wamelazimika kutoroka makwao huko al Fashir, kufuatia mapigano hayo, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN).

***VOA***

**Kufikia jana hakukuwa na tamko lolote kutoka RSF, ambalo awali lilikuwa likikanusha madai kama hayo ya kushambulia maeneo ya raia.**



## Ndumbaro mgeni rasmi mkutano Chaneta kesho

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kesho kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mchezo wa Netiboli Tanzania (Chaneta), utakaofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa Aicc jijini Arusha.

Awali, mgeni rasmi alipangwa awe Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, lakini akabadilishwa kutokana na kukabiliwa na majukumu mengine ya kitaifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chaneta, Devota Marwa, alisema maandalizi yamekamilika kuelekea kwenye mkutano huo.

„Kuanzia leo (jana), wajumbe wa mkutano huo tayari wameanza kuwasili mkoani humo kwa ajili ya kuhakikisha unafanyika kwa wakati ulipangwa," alisema Marwa.

Aidha, alisema analipongeza Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kazi kubwa linalofanya kuhakikisha gurudumu la michezo nchini linasonga mbele.

„BMT wanafanya kazi kubwa kuhakikisha kila mchezo unafanya vizuri katika mashindano mbalimbali inayoshiriki ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia," alisema.

Katika hatua nyingine aliwatakia kila kheri wachezaji wote ambao wamekwenda Paris nchini Ufaransa kushiriki mashindano ya Olimpiki.

# DODOMA FC SASA YATAMBA KUTAMBULISHA WA KIMATAIFA

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, John Kayombo, amesema bado kuna wachezaji wa viwango vya kimataifa na majina makubwa wanatarajia kuwatambulisha hivi karibuni.

Kayombo alisema mipango yao ni kumaliza msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye nafasi za juu ndio maana wanafanya usajili wa wachezaji wenye viwango vya kimataifa.

"Kwa sasa Dodoma Jiji huwezi kuifananisha na timu nyingine kutokana na usajili mkubwa tulioufanya, tupo kwenye maandalizi na mipango ya muda mrefu kuendelea kufanya vizuri ili tushiriki michuano ya kimataifa," alisema Kayombo.

Kayombo pia alimtambulisha mdhamini mkuu wa timu hiyo, PM BET na kusema wameingia mkataba wa mwaka mmoja, ambao utaanza rasmi mapema msimu mpya wa Ligi Kuu 2024/25 utakapoanza.

Tayari Dodoma Jiji wamemtambulisha kiungo mshambuliaji Ibrahim Ajibu kwa mkataba wa mwaka mmoja akitokea Coastal Union ya Tanga, beki wa kati wa kimataifa raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Heritier Lulihoshi, Dickson Mhilu na kipa Alain Ngeleka kutoka Kagera Sugar na Reliants Lusajo wa Mashujaa waliopewa mkataba wa miaka miwili.

Pia, ina benchi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Mecky Maxime, Kocha Msaidizi, Nizar Khalfan na kocha wa makipa, Manyika Peter.

Aliahidi kuingia na ushindani kwenye kila mchezo watakaocheza kwa lengo la kuwapa burudani mashabiki pamoja na wadau wa soka mkoani humo.




Watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), wakifurahia jambo jijini Dodoma juzi baada ya kuibuka washindi wa jumla na kukabidhiwa kombe katika bonanza lililojumuisha michezo mbalimbali ikiwamo mpira wa miguu, pete, riadha, bao na karata. Baaada ya ushindi huo, Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko, aliwashauri watumishi wa umma kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi ili kuimarisha afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# DRFA KUWEKEZA MIUNDOMBINU VIWANJANI

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), umesema utawekeza katika miundombinu ya viwanja kwa kuweka taa ili mpira uchezwa nyakati za usiku.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti DRFA, Lameck Nyambaya, wakati alipokuwa anazindua ligi ya vijana wenye umri chini ya miaka 13 na U-15, ya Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam.

Alisema tayari ameandaa andiko la Dar es Salaam kupata viwanja vitakavyofungwa taa kwa ajili ya mechi za usiku, na katika mradi huo atahakikisha kigamboni inaingizwa.

„Hivi karibuni nimezungumza na Rais wa TFF kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya Dar es Salaam kuwa na taa na leo (juzi), nimefika hapa nimeona kiwanja kipo sehemu nzuri, hivyo nitalifikisha kwa Rais wa TFF kwa ajili ya kufanikisha hili kwani tunataka watoto wetu wacheze mpira hapa," alisema Nyambaya.

Aidha, alisema atazungumza na Azam waweze kwenda kuangalia uwanja huo ili waweze kuweka nyasi bandia ambazo zitawekwa katika viwanja mbalimbali kikiwamo hicho cha Kigamboni.

Akibainisha changamoto ya vifaa, alisema tayari mchakato unaendelea ambapo mipira 1,000 inatarajiwa kusambazwa katika wilaya zote pamoja vifaa mbalimbali vya michezo kupitia kwa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia.

Pia aliupongeza uongozi wa Chama cha Soka Wilaya ya Kigamboni (KDFA), kwa kuandaa ligi hiyo ambayo itasaidia kuibua na kuinua vipaji vya vijana.

Alifafanua kuwa wameongea na viongozi wa timu za Simba, Yanga, Azam, JKT Tanzania na KMC, zitembelee na makocha wao waangalie vipaji vya vijana wenye umri chini ya miaka 17 na chini ya miaka 20 katika wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam.

Naye Mwenyekiti wa KDFA, Ramadhani Shauritanga, alisema wanakabiliwa na changamoto ya viwanja pamoja na timu kuwa na uhaba wa vifaa vya michezo ambavyo vinahitaji uchumi imara.

Alisema lengo la ligi hiyo ni kuwaandaa vijana ambao ndani ya miaka mitano watacheza katika Timu za Taifa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ANATAKA MKATABA

KIUNGO wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, ameiambia Manchester City kuwa anataka uhamisho wa kudumu kutoka kwa klabu hiyo, huku Everton na Aston Villa zikizingatia mkataba wa mkopo. ***(Football Insider)***

### IHENACHO KUTUA SEVILLA

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kujiunga na Sevilla baada ya mkataba wake na Leicester City kumalizika. ***(Sky Germany)***

### WILLIAMS AWANIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain bado ina nia ya kumsajili winga wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22. ***(RMC)***

### RAPHINHA ATAKIWA VILLA

ASTON Villa inataka kumnunua mshambuliaji wa Barcelona na Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa majira ya joto. (Football Insider)

### GYOKERES AGOMBEWA

KLABU za Liverpool na Tottenham Hotspur, zimeungana na Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26 kutoka Sporting Lisbon. ***(Football Insider)***

### ARSENAL KWA ALVAREZ

ARSENAL na Chelsea ziko tayari kuwania saini ya mshambuliaji wa Manchester City na Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 24. ***(TeamTalk)***

### FELIX MKATABA BADO

MKATABA kati ya Aston Villa na Atletico Madrid kumhusu mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24, haujakamilika bila pendekezo rasmi lililotumwa kwa klabu hiyo ya Hispania**. *(Fabrizio Romano)***

### THIAW EURO MILIONI 40

KLABU ya Newcastle italazimika kulipa euro milioni 40 kama wanataka kumsajili beki wa kati Mjerumani Malick Thiaw mwenye umri wa miaka 22, kutoka AC Milan**. *(Gazzetta dello Sport)***

### DOAK AVUTIA CITY

LEICESTER City na Southampton zinavutiwa na mshambuliaji wa Liverpool na Scotland, Ben Doak mwenye umri wa miaka 18, ikiwa klabu hiyo itamweka kwa mkopo. ***(Athletic)***

### VILLLA KUMUUZA DIGNE

ASTON Villa inajiandaa kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Lucas Digne, 3***1. (Football Insider)***

### UGARTE SAFI UNITED

KIUNGO wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23, amekubaliana maslahi binafsi na Manchester United, ambao wanaendelea kufanya mazungumzo na Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano)***

### MCTOMINAY AWEKEWA BEI

MANCHESTER United imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay, 27. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NDOTO YA BARCA NI KWA WILLIAMS, OLMO

Hata hivyo bado kuna foleni kubwa kuhusu usajili na wanahitaji kulipa punguzo la...

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA wanataka kumsajili kiungo mshambuliaji wa RB Leipzig, Dani Olmo, msimu huu wa majira ya joto, lakini wanajaribu kwanza kukamilisha dili la winga wa Athletic Club, Nico Williams, kwa mujibu wa 90min.

Miamba hao wa Katakunya wamekumbwa na matatizo ya kifedha katika miaka ya hivi karibuni, lakini wamekuwa na imani wazi kuhusu uwezo wao wa kufanya kazi katika soko la uhamisho wa majira ya kiangazi.

Hata hivyo, bado wana vikwazo vya kushinda - bado kuna foleni kubwa Barcelona kuhusu usajili na wanahitaji kulipa punguzo la euro milioni 100 ili kufuata sheria kali za kifedha za LaLiga.

Barca ina ndoto ya mawinga Williams na Lamine Yamal kuiga ushujaa wao wa Euro 2024 katika viwango vya klabu, huku rais Joan Laporta, Mkurugenzi wa Michezo, Deco na Kocha Mkuu, Hansi Flick, wote wakikubali kwamba yeye ndiye shabaha yao kuu ya uhamisho.

Klabu hatimaye inadhani kuna njia ya kufadhili uhamisho wa Williams ikiwa wanaweza kupata nafasi yake ya kujiunga na mradi huo.

Barcelona wanaamini kuwa Williams atakuwa tayari kupunguza mshahara wake au kuupanga kwa njia inayokidhi mahitaji yao ya kifedha kwa sasa, jambo ambalo linaweza kusababisha kupunguzwa kwa mshahara msimu huu iwapo ataondoka Athletic.

Wakati huo huo, Barcelona bado wana matumaini ya kufanya makubaliano na Olmo, kwani hapo awali walituma ofa ya mdomo kwa Leipzig ambayo iliambatana na kifungu chake cha kuruhusiwa kuondoka cha euro milioni 60, lakini kwa masharti ya malipo yakifanya mpango huo kuwa nafuu zaidi.

Kwa sasa, hakujawa na mafanikio, lakini Barca wanaweza kujaribu tena baada ya sakata la Williams kukamilika.

Leipzig bado iko wazi kwa mauzo ya Olmo kwa euro milioni 60, ndiyo maana hakuna aliyeharakisha kushinda tarehe ya mwisho ya Julai 20 kwa kifungu cha kutolewa.

Vyanzo vya habari vya Manchester City vinadai kuwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England hawamo kwenye kinyang'anyiro hicho licha ya ripoti kusema vinginevyo, lakini Manchester United na Bayern Munich wanamwaniwa.

# ENDRICK: RONALDO CHANZO KUTUA MADRID



**MADRID, Hispania**

ENDRICK amefichua kuhusu jinsi ilivyokuwa na ndoto ya kuichezea Real Madrid kwani alikuwa na mapenzi ya muda mrefu.

Kijana huyo wa Kibrazil, ambaye kuhamia kwake Bernabeu kumedumu kwa takriban miaka miwili, alikuwa na hisia kali alipokuwa amevalia jezi maarufu za rangi nyeupe kwa mara ya kwanza na kufichua kwa nini ilikuwa ni kitu alichotamani tangu akiwa mvulana mdogo.

„Sikuwa nimepanga kulia, lakini nimeipenda Real Madrid tangu nilipokuwa mdogo kwa sababu kulikuwa na mtu ambaye alikuja maishani mwangu, Cristiano Ronaldo," alisema Endrick.

„Ilikuwa ni kwa sababu yake kwamba nilivutiwa na Real Madrid. Nilitafuta picha zake muda mrefu uliopita, ikiwa ni pamoja na Emilio Butragueno. Nimekuwa nikiipenda Real Madrid. Kuichezea Real Madrid ni la aina yake kwangu."

Ronaldo aliifungia Madrid mabao 450 katika mechi 438 pekee kati ya 2009 na 2018. Endrick alikuwa hajatimiza hata umri wa miaka mitatu wakati Ronaldo alipojiunga na Madrid kwa uhamisho wa rekodi ya dunia kutoka Manchester United.

Kutakuwa na ushindani wa kupata nafasi kutoka kwa Kylian Mbappe, Vinicius Junior na Rodrygo msimu huu, lakini Endrick, ambaye amekabidhiwa jezi nambari 16 ya Madrid iliyovaliwa mara ya mwisho na Alvaro Odriozola, hana nia ya kuondoka mara moja kwa mkopo ili kuwa na muda mzuri wa kucheza.

„Kama nilivyosema, nimekuwa nikiipenda Real Madrid tangu nikiwa mdogo na ninataka kuwa hapa. Ilikuwa ndoto yangu na sikujali kitu kingine chochote," alisema.

„Nilimuuliza baba yangu ikiwa Real Madrid walikuwa kwenye mazungumzo na nikamwambia kuwa sijali kuhusu timu nyingine yoyote. Natamani kutumia Real Madrid maisha yangu yote."

## United yapata balaa ikichapwa na Arsenal

**LOS ANGELES, Marekani**

MSHAMBULIAJI Rasmus Hojlund na mchezaji mpya aliyesajiliwa kwa pauni milioni 52, Leny Yoro wote walipata majeraha kipindi cha kwanza wakati Manchester United ikipoteza mchezo wao wa kwanza wa ziara ya Marekani dhidi ya wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Arsenal kwa mabao 2-1 mjini Los Angeles juzi.

Hojlund aliipatia timu yake bao la kuongoza dakika ya 10 alipotumia vizuri pasi ya Marcus Rashford, na kumzidi ujanja mlinzi Ayden Heaven, kisha akamfunga kipa Karl Hein kwa shuti kali.

Mchezaji huyo wa Denmark alipiga pasi iliyotoka kwa Aaron Wan-Bissaka kutoka eneo la karibu kabla ya kuonekana kupata jeraha la misuli baada ya dakika 15 hali iliyomaanisha asingeweza kuendelea.

Yoro mwenye umri wa miaka miaka 18, ambaye alijiunga na United kutoka Lille siku 10 zilizopita, alihitaji matibabu ya muda mrefu kabla ya kutolewa nje.

Kwa kuzingatia idadi kubwa ya majeruhi ambayo yalimsababishia kocha Erik ten Hag msimu uliopita, kupoteza wachezaji wawili waandamizi kwa njia hiyo chini ya wiki tatu kabla ya United kufungua kampeni yao mpya ya Ligi Kuu England dhidi ya Fulham uwanjani Old Trafford mnamo Agosti 16, si jambo zuri.

„Tunapaswa kusubiri saa 24 na ndipo tutajua zaidi," alisema Ten Hag akiiambia MUTV.

„Tulikuwa waangalifu sana, haswa na Leny. Inasikitisha kwamba alilazimika kuondoka, lakini tuwe chanya na tuone kitakachotokea."

Licha ya mwanzo mzuri, matokeo hayakuwa ya kuridhisha kwa Mholanzi huyo pia. Gabriel Jesus alisawazisha jambo ambalo Ten Hag alikuwa na hakika kwamba lingekataliwa kwa kuotea, kabla ya mchezaji wa akiba Gabriel Martinelli kumkata beki wa pembeni James Scanlon mwenye umri wa miaka 17 na kufunga bao la ushindi.

## Joao Felix anukia kutua Aston Villa



**LONDON, England**

KLABU ya Aston Villa inataka Atletico Madrid kupunguza bei ya Joao Felix hadi pauni milioni 50 ikiwa wanataka kuendelea na mipango ya kumsajili kwa kudumu msimu huu wa majira ya joto.

Klabu hiyo ya West Midlands imekuwa ikihusishwa na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno katika siku za hivi karibuni huku ikienda kutafuta nyongeza ya kikosi kabla ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Vyanzo vimeiambia 90min kwamba Villa wanahisi sasa wanaweza kusonga kwa uhuru zaidi katika soko la uhamisho kutokana na mauzo ya pauni milioi 50 ya Moussa Diaby kwa Al Ittihad, na watakuwa tayari kulipa kiasi hicho, au hata kidogo zaidi, kupata mbadala bora.

Kocha Unai Emery ndiye dereva mkuu nyuma ya Villa kumtaka Felix - alikiri wazi mwaka jana kumtaka, lakini alihisi kuwa hawezi kupatikana wakati huo. Hali hii sasa imebadilika na Felix sasa yuko tayari kujiunga na Villa.

Emery anaamini zaidi kwamba Felix atafaa zaidi kwa nafasi ya namba 10 nyuma ya Ollie Watkins - nafasi inayopendekezwa na mchezaji, lakini ambayo amecheza kwa shida katika miaka ya hivi karibuni, mara nyingi badala yake inatumiwa kwenye winga.

Atletico wamedhamiria kumuuza Felix msimu huu wa majira ya joto ili kurudisha baadhi ya pauni milioni 111 walizolipa mwaka 2019.

Fedha zozote zitakazopatikana kutokana na mauzo zinaweza kutumika kumnunua Conor Gallagher wa Chelsea, huku ‚The Blues' bado wakidai ada ya pauni milioni 50.

HABARI MICHEZO

# MIL. 300/- ZAPATIKANA NBC DODOMA MARATHON, WAZIRI MKUU ASHIRIKI

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameongoza washiriki zaidi ya 12,000 wa mbio za Dodoma Marathon zilizofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma huku akiwapongeza waandaaji wa mbio hizo Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kufanikiwa kukusanya fedha kiasi cha Sh. milioni 300 zitakazoelekezwa katika kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Katika mbio hizo zilizofanyika jana na kuhusisha washiriki kutoka ndani na nje ya nchi, ilishuhudiwa washiriki kutoka Tanzania, Kenya na Uganda wakichuana vikali kwa kuibuka washindi kwenye mbio tofauti hususan zile za Km 10, Km 21 na Km 42.

Waziri Mkuu aliwaongoza viongozi mbalimbali wakiwamo wa kitaifa na viongozi wa taasisi na mashirika mbalimbali walioshiriki kwenye mbio za Kilometa tano.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi na wadau mbalimbali wa mbio hizo, Majaliwa pamoja na kuipongeza Benki ya NBC kwa mafanikio hayo, alionyesha kuguswa na ongezeko kubwa la washiriki wa mbio hizo kutoka washiriki 1,500 mwaka 2020 hadi kufikia 8,000 waliojiandikisha rasmi kushiriki mbio hizo mwaka huu. Hatua hiyo alisema inasadifu mwamko mkubwa wa wananchi kushiriki katika michezo hatua ambayo itasaidia katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo ugonjwa wa moyo, kisukari na figo.

"Mchango wa Benki ya NBC katika kuinua sekta ya michezo nchini upo wazi sana ambapo wametenga fedha zaidi ya Sh. bilioni 36 katika kufanikisha udhamini wa michezo mbalimbali ikiwamo mchezo wa mpira wa miguu. Kupitia mchezo huu wa riadha mbali na kuchochea mwamko wa mchezo husika kwa jamii, kwa mwaka huu pekee wamefanikiwa kukusanya fedha kiasi cha Sh. milioni 300 zitakazoelekezwa kufanikisha juhudi mbalimbali za kiafya kupitia agenda ya msingi ya kuokoa maisha ya mama na mtoto...hongereni sana NBC," alipongeza.

Awali, akizungumza kwenye hafla hiyo, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa kuwa mdau mkubwa wa sekta ya michezo hapa nchini kupitia jitihada zake mbalimbali, alisema ukubwa wa mashindano hayo ya




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 11.5 kwa Mwanariadha, Angelina Yumba, kutoka Tanzania baada ya kuibuka mshindi wa kwanza mbio za Km 42 za Dodoma Marathon zilizofanyika jana jijini Dodoma, zikilenga kuchangia mapambano ya saratani ya shingo ya kizazi kwa kinamama. Wanaoshuhudia ni pamoja na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto) na viongozi wengine kutoka serikalini na wadau wa mbio hizo. **MPIGAPICHA WETU**

NBC Dodoma Marathon inatoa fursa kwa mamlaka zinazosimamia mchezo huo kutumia washindi mbalimbali waliopatikana kwenye mbio hizo kuliwakilisha taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa yakiwamo ya Olimpiki na yale ya Jumuiya ya Madola (Commonwealth).

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema kiasi cha Sh. milioni 300 kilichokusanywa kupitia mbio kitaelekezwa katika kufanikisha malengo ya mbio hizo ambayo ni kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road pamoja na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga kupitia Taasisi ya Benjamin Mkapa, lengo kuu likiwa ni kuboresha afya ya mama na mtoto.

Katika mbio hizo ilishuhudiwa Mwanariadha kutoka Uganda Akanswa Mingichi akiibuka mshindi wa kwanza wa mbio za Km 42 (Full Marathion) kwa upande wa wanaume baada ya kutumia muda wa saa 2 na dakika 13 akifuatiwa na Mwanariadha Eyenali Paul kutoka Kenya aliyetumia muda wa saa 2 na dakika 14 huku kwa upande wa wanawake mbio hizo ilishuhudiwa Mwanaridha Angelina Yumba akiibuka mshindi wa kwanza baada ya kutumia muda wa saa 2 na dakika 33 akifuatiwa na Chopsiriri Tufena kutoka Kenya aliyetumia muda wa saa 2 na dakika 34.

Washindi wa kwanza kwenye mbio hizo za Km 42 waliondoka na zawadi ya fedha taslimu Sh. milioni 11.5 na vifaa vya michezo kwa jinsia zote huku washindi wa pili wakiondoka na Sh. milioni tano na vifaa vya michezo kwa jinsia zote mbili.

Kwa upande wa mbio za Km 21, wanaume ilishuhudiwa Mwanariadha kutoka Kenya Peter Mwangi akiibuka mshindi wa kwanza baada ya kutumia muda wa saa 1:2:23 akifuatiwa na Mwanariadha Joseph Panga kutoka Tanzania aliyetumia muda wa saa 1:02:35 huku kwa wanawake ikishuhudiwa mwanariadha Sarah Makera akiibuka mshindi wa kwanza baada ya kutumia muda wa saa 2 na dakika 10 akifuatiwa na Suzana Chembui kutoka Kenya aliyetumia muda wa saa 1 na dakika 11.

Washindi wa kwanza kwenye mbio hizo za Km 21 waliondoka na zawadi ya fedha taslimu Sh. milioni 5.5 na vifaa vya michezo kwa jinsia zote huku wa pili wakiondoka na Sh. milioni 2.5 na vifaa vya michezo kwa jinsia zote mbili.

# Djuma aibukia Namungo FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo, imetangaza kumsajili beki wa zamani wa Yanga na AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Djuma Shaaban, ambaye atatumikia timu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano mbalimbali, ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, imeeleza usajili wa mchezaji huyo ni moja ya mapendekezo ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera ili kukiboresha kikosi hicho kuelekea msimu ujao. Imeeleza tayari mchezaji huyo ameshafika Rungwa mkoani Lindi na ameanza mazoezi ya maandalizi ya msimu ujao wa mashindano.

Awali, beki huyo wa kulia alitajwa kuwa angejiunga na Coastal Union, ambapo Ofisa Habari wa klabu hiyo, Abbas El Sabri, alithibitisha kuwa walikuwa kwenye mazungumzo kwa ajili ya kuisaidia timu yao katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Mpaka anajiunga na timu hiyo, Djuma hakuwa na klabu yoyote, lakini alichezea Yanga kuanzia 2021 hadi 2023, ambayo ilimsajili kutoka AS Vita Club ya DR Congo. Mbali na mchezaji huyo, Namungo pia imetangaza kupata saini wa kiungo wa zamani wa Yanga, Rafael Daudi Loti na Mubarak Amza Ngamchiya, wote kutoka Singida Fountain Gate.

Msimu uliopita Namungo ilimaliza ligi ikiwa nafasi ya sita, kwa pointi 36, ikicheza mechi 30, kushinda nane, sare 12 na kupoteza mechi 10, ikifunga mabao 27 na kuruhusu 29.

## Yanga SC yainyosha Kaizer Chiefs na Nabi

INATOKA UK. 24

kabla ya kwenda mapumziko lililowekwa ndani ya kimia na Aziz Ki, akipata pasi elekezi kutoka kwa Clement Mzize.

Bao hilo nalo lilitokana na uzembe wa mabeki wa Kaizer Chiefs, safari hii beki wa kushoto, Given Msimango, ambaye alikuwa na uwezo wa kuondoa mpira kwenye hatari akaleta madoido ya kutaka kupiga chenga, lakini alinyang'anywa na kufungwa bao la pili.

Alikuwa ni Mzize, ambaye baada ya kutoa pasi, safari hii aliukwamisha wavuni dakika ya 56, kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Dube.

Makosa mengine ya mabeki, yalisababisha Aziz Ki kuuwahi mpira uliorudishwa kizembe nyuma na kuujaza wavuni dakika ya 62.

Yanga imemaliza mechi zake tatu maalum nchini humo, ikishinda mbili na kupoteza moja, ambapo ilichapwa mabao 2-1 dhidi ya FC Augsburg ya Ujerumani, uliochezwa Julai 21, kabla ya kushinda kwa bao 1-0 katika mchezo wa pili dhidi ya wenyeji TS Galaxy, Jumatano iliyopita.

Katika hatua nyingine Klabu ya Yanga imesema suala ya straika, Jean Baleke, limefanyiwa kazi na huenda akatambulishwa rasmi wakati wowote.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema jana kuwa, kulikuwa na mambo ambayo yalikuwa yakishughulikiwa kabla ya kumtangaza rasmi, lakini baada ya kuweka mambo sawa, huenda akatangazwa baada ya mechi ya jana dhidi ya Kaizer Chiefs, kabla ya kilele cha Wiki ya Mwananchi, Agosti 4, mwaka huu.

„Kuhusu suala lake shughuli imemalizwa, tunaamini sasa atashirikiana vizuri na wenzake pale mbele kuhakikisha kunakuwa na kikosi imara msimu ujao," alisema Kamwe.

## Simba yajiondoa kwa Mpanzu, kipa wa Horoya atua

INATOKA UK. 24

Kutokana hilo, mchezaji huyo anatarajiwa kutimkia Klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji baada ya dili hilo kushindikana.

Wakati hayo yakiendelea, golikipa mpya wa timu hiyo, Moussa Panpin Camara, alitarajiwa kutua nchini jana mchana kwa ajili ya kusaini mkataba wa kujiunga na timu hiyo.

Picha zilizotolewa jana na vyombo vya habari na mitandaoni nchini Guinea, zilimwonyesha akiwa na mabegi yake Uwanja wa Ndege nchini humo tayari kwa safari ya kuja nchini.

Kipa huyo wa Timu ya Taifa ya Guinea, anatokea Klabu ya Horoya FC nchini humo, na anakwenda kuchukua nafasi ya Ayoub Lakred ambaye taarifa zinaeleza aliumia akiwa kwenye maandaliazi ya msimu mpya nchini Misri.

Michezo
Nipashe Jumatatu Julai 29, 2024

## Ndoto ya Barca ni kwa Williams, Olmo

UKURASA 21






Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya, akimiliki mpira dhidi ya kiungo mshambuliaji wa Kaizer Chiefs, Yusuf Maart, kwenye mechi ya Kombe la Toyota iliyopigwa katika Uwanja wa Bloemfontein, Afrika Kusini jana. Yanga ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga SC yainyosha Kaizer Chiefs na Nabi

## ●●● Yabeba Kombe la Toyota, Dube, Aziz Ki wa moto, yamaliza pia utata wa Baleke...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Soka Tanzania Bara, Yanga, wametwaa Kombe la Toyota, ikiwa ni taji lao la kwanza msimu huu, baada ya kuwabamiza wenyeji wao, Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini mabao 4-0, katika mechi maalum ya kimataifa, iliyochezwa katika Uwanja wa Bloemfontein nchini humo.

Yalikuwa ni mabao mawili ya kiungo mshambuliaji raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, Mzimbabwe, Prince Dube na Mtanzania, Clement Mzize ambayo yalitosha kuwasambaratisha wenyeji hao na waandaaji wa kombe hilo walioukuwa wakicheza mbele ya mashabiki wao.

Ilikuwa pia ni vita kwa makocha wawili waliopokezana kijiti katika timu ya Yanga, Miguel Gamondi raia wa Argentina na Nasreddine Nabi kutoka Morocco ambaye kwa sasa ndiye Kocha Mkuu wa timu hiyo ya Afrika Kusini.

Gamondi aliyeichukua timu kutoka kwa Nabi, hakumpa nafasi mwenzake ya kuonyesha chochote uwanjani, badala yake safu yake ya ulinzi ya Kaizer Chiefs ilionekana kufanya makosa mengi, yaliyozaa mabao manne.

Kama alivyofanya katika mechi dhidi ya TS Galaxy, Prince Dube alipachika bao dakika ya 24 akitumia makosa ya mabeki wa Kaizer Chiefs kujichanganya wenyewe wakati wakitaka kuokoa mpira.

Mpira huo ulianzia kwa faulo iliyopigwa na Aziz Ki, baada ya Nickson Kibabage kufanyiwa madhambi, ambao uliokolewa, lakini ukarudishwa tena kwenye lango la Wasauzi hao na kuwakuta mabeki wa timu hiyo wawili wote waliokuwa wanataka kuokoa mpira, wakachanganyana na kumpa nafasi Dube aliyeukuta mpira upo mbele yake, akapiga shuti dhaifu la ufundi mkubwa uliompoteza maboya, kipa Brandon Petersen na kujaa upande wake wa kulia.

Kama angekuwa makini, Ranga Chivaviro, angeweza kuisawazishia Kaizer Chiefs bao dakika ya 30, baada ya kupasiwa mpira akiwa ndani ya eneo la hatari, lakini aliumiliki vibaya na ukasogea mbali zaidi na kabla hajaufikia, Dickson Job alitokea na kuufagia.

Golikipa, Djigui Diarra alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika tatu kabla ya kwenda mapumziko alipodaka shuti la kushutukiza lililopigwa na Mfundo Vilakazi.

Yanga ilipata bao la pili sekunde chache

INAENDELEA UK. 23

## Simba yajiondoa kwa Mpanzu, kipa wa Horoya atua

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imejiondoa kwenye dili la kutaka kumsajili winga wa AS Vita Club, Elie Mpanzu, kwa kile ilichobaini kuwapo kwa udanganyifu mwingi, huku mchezaji huyo sasa akijiandaa kutimkia Ubelgiji kwenye Klabu ya KRC Genk.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema viongozi wa Simba wameamua kukata mawasiliano baada ya kuwapo kwa watu wengi wanaojitaja kama mameneja, huku kila mmoja akidai ndiye mwenye mamlaka na mchezaji huyo, kitu ambacho kimesababisha kuchelewa kumsajili na kujiunga na wenzake kambini nchini Misri.

„Viongozi wa Simba wamefanya kila jitihada, dili lilikuwa likamilike zamani sana, kama utakumbuka awali ilipeleka ofa ya dola 200,000 za Kimarekani, lakini klabu yake ilikataa na ikahitaji 250,000.

„Viongozi hawakuendelea na dili hilo, lakini baada ya kuondoka kwa Kibu Denis walirejea tena na kiasi ambacho alihitaji mara ya pili, lakini bado kumekuwa na mkanganyiko, klabu inahitaji pesa, klabu yake ambayo alianzia kucheza soka nao wanahitaji.

„Pia kuna mameneja kadhaa ambao baada ya kuona dili hilo nao wamejitokeza, sasa viongozi wameamua kuwakatia simu wote, ukweli ni kwamba usajili wa Mpanzu una uongo mwingi, msimamizi halali wa Mpanzu hajulikani, hivyo wamekwepa matatizo,“ kilisema chanzo hicho.

Chanzo hicho kimesema huenda Simba wakaingia tena sokoni kusaka winga wa kulia kuziba nafasi ya Kibu ambaye ametorokea nchini Norway, huku suala lake likionekana haliwezi kumalizika hivi karibuni kwani kama si kumuuza bei inayotaka klabu hiyo, basi kutoa adhabu kwa mchezaji na kuishtaki klabu iliyomrubuni.

Habari zinasema tayari Mpanzu alishakubali kujiunga na Simba aliyetarajiwa kulipwa mshahara wa Sh. milioni 26 za Kitanzania na ada ya usajili Sh. milioni 323 za Kitanzania.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >